# Nipashe

Alhamisi Oktoba 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580355

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**MAGUFULI** aahidi ujenzi shule za sekondari za sayansi mikoa yote 26

UKURASA 2



**LISSU** aibuka na utetezi mzito mbele ya Kamati ya Maadili ya Uchaguzi

UKURASA 2

# NEC yasema hakuna muda zaidi kampeni

**NI** kwa wagombea ubunge walioshinda rufani baada ya kuenguliwa... *Endelea uk. 2*



"Rais Magufuli amefanya mambo makubwa na anapaswa kupewa nafasi tena. Ninamuunga mkono katika urais, wananchi wanipe mimi ubunge."

**Mrema**



"Kwa kushirikiana na wadau wengine tunakamilisha mchakato wa kuanzisha mfuko wa wajasiriamali Vunjo."-

**Kimei**



"Shule hizo zitakuwa za bweni na watoto wetu hasa wa kike watapata muda mwingi wa kusoma, lazima watoto wetu wote wapate elimu."-

**Kiwelu**



"Ndani ya miezi miwili, barabara korofi ya kwenda Kochakindo itakuwa imejengwa na kuunganishwa na vijiji vingine."-

**Mbatia**

# Miamba minne inayotikisa ubunge jimboni Vunjo

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### ACT - WAZALENDO YAAHIDI KUBORESHA BANDARI MTWARA

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama hicho kitahakikisha kinaimarisha...

UKURASA WA 4

### KESI YA KUPINGA MUUNGANO YATUPWA

MAHAKAMA ya Haki ya Afrika Mashariki, imetupilia mbali kesi iliyokuwa ikihoji na kupinga uhalali wa vifungu na hati ya makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar baada ya...

UKURASA WA 5

### BODI YAONGEZA MUDA MAOMBI MIKOPO ELIMU

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)...

## Ofisa TRA kortini madai ya rushwa

UKURASA 4

**MICHEZO** AZAM ANGA MOJA NA SIMBA, YANGA UK 24

MAONI, KATUNI UK. 6



Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli, akihutumia maelfu ya wananchi katika mkutano wa kampeni uwanja wa Airport, jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**

# Walioshinda rufani kutopata nyongeza muda wa kampeni

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema haitaongeza muda wa kampeni kwa wagombea ubunge walioshinda rufani dhidi ya mapingamizi na kurejeshwa.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, kupitia tangazo la tume lililotolewa katika vyombo vya habari jana.

Katika tangazo hilo, NEC iliujulisha umma kuwa Septemba 28, ilikamilisha kupokea, kuchambua na kuamua rufani zote zilizowasilishwa na kupokelewa kutoka kwa wasimamizi wa uchaguzi.

Tangazo hilo lilieleza kuwa rufani za wabunge mpaka wanakamilisha zilifikia 165 na kati yao waliorejeshwa ni baada ya uamuzi ni 67, wanaoendelea na uteuzi baada ya uamuzi wa rufani ni 59 na ambao hazikufanikiwa ni 39.

Dk. Mahera alipoulizwa kama NEC itawaongezea muda wagombea ambao rufani zao zilitoka wakati wengine wakiendelea na kampeni majimboni, alisema hawana mpango huo.

"Umefanya utafiti wa wabunge au madiwani ambao hawajaanza kampeni mpaka sasa, na hawakuwa na rufani, kuna watu wengi hawajaanza kampeni.

"Hawa wenye rufani kutokuanza ndiyo iwe suala la kuongelea?" Alihoji na kuendelea: "Kwa kifupi hakuna kuongeza muda, na bado wana muda na kuna watu ambao bado hawajaanza kampeni."

Katika tangazo la NEC, miongoni mwa wagombea 67 waliorejeshwa jimboni kwenye mabano ni Boniface Jacob CHADEMA (Ubungo), Devota Minja CHADEMA (Morogoro Mjini) na Fanuel Mkisi CHADEMA (Vwawa).

Wengine ni Hamad Kamtande CHADEMA (Liwale), Iddi Kizota CHADEMA (Kondoa Mjini), Mtutura Abdallah ACT-Wazalendo (Tunduma Kusini), Mgawe Stanley CHADEMA (Kibamba), Mussa Mbarouk CUF (Tanga Mjini) na Yosepher Komba CHADEMA (Muheza).

Tangazo hilo lilitaja orodha ya wagombea ubunge 59 ambao wanaoendelea na uteuzi baada ya uamuzi wa rufani ambapo baadhi yao ni Makame Mbarawa CCM (Mkoani), Hamis Mwijuma maarufu Mwana FA CCM (Muheza) na Deogratus Mwanyika CCM (Njombe Mjini).

Wengine ni Patrick Ndakidemi CCM (Moshi Vijijini), Abdallah Ulega CCM (Mkuranga), Edwin Swalle CCM (Lupembe), Jumanne Miraji CCM (Singida Mashariki) na Elibariki Kingu CCM (Singida Magharibi).

Kwa upande wa wagombea ubunge ambao rufani zao hazikufanikiwa baadhi yao ni Amina Abdul-Rahiman CHADEMA (Bahi), Msabaha Rajabu CUF (Kilosa) na Fredrick Kihwelo CHADEMA (Mafinga Mjini).

**■Imeandikwa na Romana Mallya na Evelineneena Ernest, (SJMC)**

# JPM aibuka na shule ya sayansi kila mkoa

**Na Gwamaka Alipipi,** MBEYA

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali atakayoiongoza itajenga shule 26 za mchepuo wa masomo ya sayansi, shule moja kwa kila mkoa.

Vilevile, ameahidi kuwa shule 1,500 za sekondari nchini zitaunganishwa na huduma ya intaneti na kupatiwa vifaa vya kufundishia masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alitoa ahadi hiyo jana mkoani Mbeya alipozungumza na wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza kwenye uwanja wa ndege wa zamani kumsikiliza aliponadi sera zake na kuwaomba kura ili aendelee kuwa Rais wa nchi.

"Pia, tutaendelea kutoa huduma ya elimu bure, kujenga shule 26, kila mkoa shule moja kwa ajili ya mchepuo wa sayansi ili kusaidia sayansi, TEHAMA na Hisabati katika mikoa yetu.

"Tutaziunganisha shule za sekondari 1,500 kwa intaneti na kuzipatia vifaa vya kufundishia TEHAMA ikiwamo compyuta," alisema mgombea huyo.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, walimu zaidi ya 20,000 pia watapewa mafunzo ya masomo ya hisabati, sayansi na lugha, lengo kuu likiwa kuongeza wataalamu wa sayansi nchini.

Dk. Magufuli alisema serikali pia itaendelea kuimarisha masomo ya ufundi, ikiwamo kuvihimiza vyuo vikuu nchini kuendelea kuchukua wanafunzi wengi.

Kuhusu sekta ya afya, Dk. Magufuli alisema serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu ya hospitali ya Kanda ya Mbeya.

"Tutakamilisha ujenzi wa jengo la kisasa la mama na mtoto katika hospitali ya wazazi Meta iliyopo Mbeya ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia kinamama 200 kwa wakati mmoja.

"Itakuwa na vyumba vya upasuaji, wodi ya wagonjwa mahututi, wodi ya kujifungulia, mradi huu utagharimu Sh. bilioni 9.2," alisema Dk. Magufuli.

Mgombea huyo pia alisema katika miaka mitano ijayo, serikali itaimarisha huduma za kibingwa katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya, itakayokuwa na uwezo wa kutibu magonjwa ya moyo, figo na saratani.

Alisema Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Wilaya zitaboreshwa na kuwa na uwezo wa kupokea wagonjwa kutoka nchi za jirani.

Kuhusu maji, Dk. Magufuli alisema serikali itatekeleza miradi mikubwa miwili ya maji mkoani Mbeya itakayokuwa na thamani ya Sh. bilioni 41, mmoja utajengwa Lujewa ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 30 na mwingine wilayani Chunya kwa gharama ya Sh. bilioni 11.

Dk. Magufuli pia alibainisha miradi anayojivunia kwa kutekelezwa na serikali chini ya uongozi wake ikiwamo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya na elimu.

# Lissu aibuka na utetezi wito Kamati ya Maadili

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema hadi sasa hajapokea barua ya kuitwa kuhojiwa kwenye Kamati ya Maadili kama inavyodaiwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kutokana na hali hiyo, Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, amesema anaendelea na ratiba ya mikutano yake ya kampeni kama kawaida.

Akiwa Arusha Septemba 27, mwaka huu, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Wilson Mahera, alisema tume imemwita Lissu kwenye Kamati ya Maadili kujibu tuhuma ya kwamba Rais John Magufuli alikutana jijini Dodoma na wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya majimbo kwa lengo la kuhujumu uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Mkurugenzi huyo wa NEC alisema walimwandikia Lissu barua ya kufika kwenye kamati hiyo Septemba 29 mwaka huu ili kujibu tuhuma hizo.

Hata hivyo, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Arusha jana kuhusu tathmini na mwenendo wa mikutano yake ya kampeni, Lissu alisema hajapokea barua ya kuitwa kwenye kamati hiyo na hivyo hawezi kwenda pasi na kuwapo na wito.

"Ndugu waandishi, ninadhani mtakuwa mmesikia na kusoma kwenye mitandao ya kijamii Mkurugenzi wa Uchaguzi akisema mimi nimeitwa kwenye Kamati ya Maadili, mimi pia taarifa hizo nimeziona mitandaoni kwamba kuna malalamiko kutoka CCM na Chama cha NRA kwamba nimekiuka kanuni za maadili ya uchaguzi, "Kwa mujibu wa kanuni za maadili ya uchaguzi mkuu, kama ni kweli kwamba kuna malalamiko yoyote dhidi ya mgombea kwenye kampeni, malalamiko hayo yanatakiwa kutolewa kwa maandishi kwa muhusika kwa kuwa yeye ndiyo mlalamikiwa,"aliongeza Lissu.

"Kwa kuwa mimi ndiyo mlalamikiwa walitakiwa kuniletea malalamiko hayo kwa maandishi kwa kuwa ninadaiwa kukiuka maadili ya uchaguzi na ambaye nilisaini maadili hayo.

"Kwa mujibu wa maadili haya, ni mimi pekee ninayetakiwa kuletewa hayo malalamiko na pia mimi mwenyewe ndiyo ninatakiwa kuyajibu kama yapo. "Hadi hapa nilipo leo (jana) na tangu mmeanza kusikia hizo taarifa za kuitwa kwenye kamati ya maadili, sijaona mtu yeyote wala ofisa yeyote kutoka tume amenifuata kuniletea taarifa ya maandishi kuhusu tuhuma zinazodaiwa.

"Ninasema tena, kama kweli mimi ni mlalamikiwa, kanuni za maadili zinasema mlalamikiwa huyo aandikiwe malalamiko yake na akabidhiwe, mpaka sasa sijaona malalamiko yoyote wala wito wowote. Kwa hiyo, sisi tunaendelea kusonga mbele.

"Tume ina wajibu wa kufuata sheria na kanuni na yenyewe na haipo juu ya sheria. Hizi kanuni zimetengenezwa na tume yenyewe na sisi tulilazimika kuzisaini kama unataka kugombea na usiposaini, hugombei," alisema.

Alisema hadi sasa CHADEMA wameshafanya mikutano mikubwa yenye mafanikio katika mikoa ya Iringa, Pwani, Kagera, Mwanza, Geita, Njombe, Mbeya, Dodoma, Morogoro, Songwe, Katavi, Rukwa, Kigoma na Mara.

"Katika mikutano yetu ya kampeni, Watanzania wako tayari kufanya mabadiliko na sehemu zote tulizokwenda tumepokewa na maelfu ya watu, wananchi wamekuja kwa mapenzi yao, hatukusafirisha watu kwenye malori," Lissu alitamba.Katika taarifa yake ya jijini Arusha, Dk. Mahera alisema barua hiyo ilishawasilishwa kwenye makao makuu ya CHADEMA na Kamati ya Maadili itasikiliza tuhuma hizo wiki hii jijini Dar es Salaam.

**■Imeandikwa na Allan Isack na Cynthia Mwilolezi**

# Miamba minne yaibua mtikisiko Vunjo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NI pagumu. Hawana desturi ya kumpa mgombea kura za kishindo, zaidi ya wapigakura kuamua nani aongoze Jimbo la Vunjo mkoani Kilimanjaro kwa muhula mmoja tu wa miaka mitano, ndivyo ambavyo inaweza kuelezwa.

Ndivyo inavyoonekana kwa sasa kutokana na kuwapo kwa vita isiyo na damu kati ya Mwenyekiti wa Taifa wa NCCR Mageuzi, James Mbatia, ambaye ni mbunge aliyemaliza muda wake na Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Vita hivyo vya kuwania kiti cha ubunge katika jimbo hilo vinanogeshwa zaidi na mwanamke pekee, Grace Kiwelu (CHADEMA), ambaye amekaa bungeni kwa miaka 20 akiwa mbunge wa Viti Maalum. Pia katika kinyang'anyiro hicho, yumo nguli wa siasa, Augustino Mrema, Mwenyekiti wa Taifa wa Tanzania Labour Party (TLP).

Joto la kisiasa katika jimbo hilo, linazidi kupamba moto wakati wanasiasa hao wakitifuana jukwaani na tambo, kutoa ahadi na kuzuka kwa vituko vya kila aina.

Katika kampeni zake, Dk. Kimei amekuwa akitafuta kura kwa kuwaeleza wananchi wa jimbo hilo kwamba wakimpa ridhaa na kushinda katika uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu, atapambana kufa na kupona mji wa Himo utangazwe kuwa makao makuu ya wilaya ya Moshi.

Wakati wa uzinduzi wa kampeni Septemba 12, Dk. Kimei alisema uamuzi wake wa kugombea ubunge unatokana na changamoto nyingi jimboni humo ikiwamo miundombinu mibovu ya barabara, elimu, afya na ukosefu wa masoko thabiti kwa mazao.

Pia aliahidi kwamba atatumia uzoefu wake katika sekta ya fedha, kuanzisha mfuko wa ujasiriamali wa jimbo ambao utahusika kutoa mikopo nafuu kwa wananchi, ili kuwapa mitaji na hivyo kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajiri ili kuwapaisha kiuchumi.

"Kwa kushirikiana na wadau wengine tunakamilisha mchakato wa kuanzisha mfuko wa wajasiriamali Vunjo. Mimi mwenyewe nitatoa andiko la mradi ili kupata fedha za uwezeshaji wa makundi maalum ya wakulima, wafugaji, vijana, wanawake, bodaboda na mafundi makenika kwa kuwapa mikopo nafuu.

**MBATIA ATESWA NA REKODI**

Mgombea wa NCCR Mageuzi, Mbatia, mwanasiasa mwenye ushawishi na mtu mwenye uwezo wa kujenga hoja, anaungwa mkono na kundi kubwa la viongozi wa dini.

Ushawishi wake na mbinu nyingi anazotumia kutaka kuwashinda wapinzani wake, zinampasua kichwa, hasa anapowaza namna ya kuvunja rekodi ya wapigakura wa Vunjo ili wamrejeshe tena kwa vile jimbo hilo halina historia hiyo tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi.

Katika uzinduzi wa kampeni Septemba 19, alitumia urafiki wake wa karibu na Rais John Magufuli kama turufu kueleza, namna Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilivyoumaliza mkwamo wa miradi ya ujenzi wa barabara za jimbo hilo uliokuwa umeingiliwa na itikadi za kisiasa.

Mbatia anawaomba wakazi wa Vunjo kumchagua tena kwa kipindi cha pili mfululizo kuwa mbunge wao, akiahidi katika muda wa miezi miwili kuanzia sasa, moja ya barabara korofi ya kwenda Kochakindo itakuwa imejengwa na kuunganishwa na vijiji vingine ili kufungua fursa ya usafirishaji kufika mji wa Himo.

**KIWELU KATIKATI YA MSITU**

Huyu ni mwanamke pekee ambaye ni muumini wa siasa za kistaarabu aliyejitokeza kuvunja mwiko wa utamaduni wa Wachaga, akiwa mwanamke aliyethubutu kugombea kiti cha ubunge Jimbo la Vunjo.

Amekomaa katika siasa za kiharakati, ana ushawishi lakini ni mtu aliyewekeza Vunjo kisiasa kwa zaidi ya miaka mitano, akijijenga ili kupindua meza na kuwa mbunge wa kwanza mwanamke kuliongoza jimbo hilo.

Ameelekeza akili yake na nguvu zake kuhuisha mfumo wa elimu na afya katika jimbo hilo kama atachaguliwa.

Katika ahadi zake kwenye mikutano ya kampeni inayoendelea, Kiwelu ameahidi kutatua tatizo la ubovu wa miundombinu ya madarasa mengi katika hilo ikiwa atachaguliwa.

"Shule nyingi zilizoko katika jimbo letu la Vunjo ni chakavu, lakini hakuna walimu wa kutosha kwenye shule zetu. Baadhi ya kata wananchi wanachangishwa fedha za kwenda kulipa walimu.

"Niwahakikishie katika miaka mitano ijayo kama mtanichagua kuwa mbunge wenu, kwa kushirikiana nanyi na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi pamoja na wadau mbalimbali, tutajenga Shule ya Sekondari Riweni, Matala na Mariale.

"Niwahakikishie nitajitahidi kadri ya uwezo wangu na ninamuomba mwenyenzi Mungu anisaidie, shule hizo zitakuwa za bweni na watoto wetu hasa wa kike wapate muda mwingi wa kusoma na mimi kama mama ninajua uchungu wa mtoto, lazima watoto wetu wote wapate elimu," alisema.

**MREMA NA KIKI YA JPM**

Augustino Mrema anafanya kampeni zake chini kwa chini, ana historia Vunjo na kitendo chake cha kumuunga mkono Rais John Magufuli anakitumia kama turufu ya kutafuta kura ili kuwapiku washindani wake.

Anajua wapigakura wengi hivi sasa wana imani kubwa na Rais Magufuli kutokana na matokeo chanya ya kazi zake hasa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kama Stiglers Gorge, Reli ya Kisasa (SGR) na ufufuaji wa reli ya kaskazini iliyokufa miaka 16 iliyopita.

Mrema kuteuliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole kwa kipindi cha pili, 2020/2023 ni heshima kubwa aliyopewa na Rais Magufuli na kaingia kugombea ubunge bado kashikilia cheo alichopewa na Rais.

Wakati uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi unafanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1995, Mbatia alishinda ubunge katika jimbo hilo lakini hakurudi tena katika uchaguzi wa mwaka 2000.

Alipokonywa kijiti hicho na Meja Mstaafu Jesse Makundi (TLP) mwaka 2000 ambaye na yeye alipoteza nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 mbele ya Alloyce Kimaro.

Wananchi wa Vunjo walimchagua Augustino Mrema katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 hadi 2010, kuwa mbunge wao, lakini hata yeye alishindwa kufurukuta kupata kipindi cha pili.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Mbatia alirejea Vunjo na kupata tena ubunge aliodumu nao mpaka mwaka huu.

# ACT yaahidi kuimarisha Bandari Mtwara

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema kuwa chama hicho kitahakikisha kinaimarisha Bandari ya Mtwara ili kuhudumia korido ya maendeleo ya Mtwara (Mtwara Corrior).

Pia, kitafungua fursa za biashara kwa wananchi wa mikoa na wilaya za mpakani ikiwamo kunufaika na biashara za pande zote.

Akizungumza na wananchi wa Jimbo la Tunduru, wakati wa mkutano wa kampeni za mgombea ubunge wa jimbo hilo, Ado Shaibu, alisema ni lazima kuhakikisha fursa zinanufaisha wananchi wote wa maeneo hayo.

Alisema kuimarishwa kwa bandari hiyo inayohusisha mradi wa Mchuchuma na Liganga na kuwezesha kusafirisha bidhaa kutoka nchini Malawi na Kaskazini mwa Msumbiji.

Kwa mujibu wa Zitto, miradi hiyo na bandari hiyo itasaidia kuufanya mji wa Mtwara kuwa kituo cha huduma kwa miradi ya uwekezaji wa mafuta na gesi Kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji.

"Tutahakikisha tunajenga mahusiano mazuri ya kimataifa, Tunduru ilihifadhi wapigania uhuru...mikoa ya mipakani na wilaya za mipakani zina fursa za maendeleo," alisema na kuongeza:

"Tunataka kufungua soko kati ya Kaskazini mwa Msumbiji na wilaya za Kusini kama Tunduru, tunataka watu wafanye biashara, mzunguko wa fedha uongezeke kama mwenzetu ana matatizo tusaidiane, tushirikiane kutatua," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Zitto, wana Tunduru hawajanufaika na uwepo wa mpaka na kwamba chama hicho kimeona fursa na kwa kutumia Jumuiya ya SADC kujenga mahusiano mazuri.

Alisema ACT-Wazalendo itahakikisha inajenga uhusiano na ushirikiano baina ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji ikiwamo kutumia fursa za maendeleo.


NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

**Advertisement on Business Opportunities**

**INFORMATION ON BUSINESS OPPORTUNITIES**
**Date: 1st October 2020**
**Reference no: 03/NCA/2020**
**Subject: Provision of Consultancy Services**
**Contracting Authority: Norwegian Church Aid Tanzania**
**Deadline for submission of letter of interest: 8th October 2020**

**Background**
Norwegian Church Aid (NCA) is a Norwegian non-governmental and development organization working to promote Social Justice, Human Rights and Economic Justice for poor communities. NCA has its foundations based in the congregation of Churches in Norway, whose efforts are dedicated towards eradicating poverty, its causes and social deprivation. In Tanzania, NCA works in collaboration with local faith-based partners (FBOs)

Norwegian Church Aid Tanzania, in cooperation with its partner invites qualified individual consultants or firms in provision of the following services to respond to this advertisement.

Consultants who have responded to this advertisement and provide the required information will be shortlisted and the qualified ones will receive a Request for Proposal **(RFP)** in providing the following Consultancy services:

1. Close Technical Supervision for the ongoing work of Drilling of Six Boreholes in selected villages in Hanang and Mbulu Districts and issue a certificate of completion.
2. Preparation of Tender Document for Construction and Installation of Six Solar Micro Water Yard Towers within the selected villages in Hanang and Mbulu Districts and issue a certificate of completion.

The interested Consultants shall provide the following information to the Contracting Authority using the contact details below:

- Indicate which Consultancy service you are interested in.
- Provide the following information:
  - the individual or company's name and contact details;
  - contact person;
  - CV of individuals or brief description of the company's background and main line of work; and
  - experience with this kind of service.

**This is purely information on business opportunities and does not constitute a commitment to purchase or any other form of contractual commitment with the Contracting Authority.**

Norwegian Church Aid will not accept hard copy of profiles, therefore all documents in original should be scanned in PDF and should be sent to <u>Procurement.Tanzania@nca.no</u> where the shortlisting will be done by the Procurement Committee and successful candidates will be contacted.

115924502

# Ofisa TRA kortini tuhuma za rushwa

**Na Richard Makore,**
MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, imemfikisha mahakamani Ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mary Moyo, kwa tuhuma za kuomba rushwa.

Moyo anadaiwa kuomba rushwa ya Sh. milioni nane kutoka kwa mfanyabiashara ili amrekebishie hesabu za deni alilokuwa anadaiwa kutoka Sh. milioni 97 hadi Sh. miliomi 35.

Mtuhumiwa huyo, alifikishwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza na kusomewa mashtaka mawili, ambayo ni kuomba rushwa kutoka kwa mfanyabiashara wa mkoani Mwanza, Laurent Kahozy na kupokea rushwa ya Sh. 60,000.

Kesi hiyo ilifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Monica Ndyekobora na kusomewa mashtaka hayo na Wakili wa Serikali, Moses Malewo.

Malewo alidai kuwa mtuhumiwa aliomba rushwa kinyume cha kifungu cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Aidha, ilidaiwa kuwa mtuhumiwa alikubaliana na mfanyabiashara huyo, kwamba akimpatia kiasi hicho cha fedha angemtengenezea hesabu na kupunguza deni hilo.

Malewo ambaye ni Ofisa wa TAKUKURU, alidai kuwa kwa nyakati tofauti mfanyabiashara huyo aliambiwa kuwa anadaiwa kiasi kikubwa cha deni la kodi, ambacho hakuwa na kumbukumbu nacho.

Baada ya taarifa hiyo, mfanyabiashara huyo aliandikiwa barua na TRA inayoonyesha kuwa anadaiwa Sh. milioni 97.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Oktoba 21, mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani hapo na mtuhumiwa yuko nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamdun, akimjulia hali mwalimu wa Sekondari ya Kiranyi wilayani Arumeru, Veronica Kidemi, aliyelazwa Hospitali ya Selian, anayedaiwa kukatwa kiganja cha mkono wa kulia na kutenganishwa na mkono wake kwa panga na mumewe. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Kesi kupinga Muungano yatupwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Haki ya Afrika Mashariki, imetupilia mbali kesi iliyokuwa ikihoji na kupinga uhalali wa vifungu na hati ya makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar baada ya kukubali pingamizi la awali walalamikiwa.

Kadhalika, mahakama hiyo iliyoketi chini ya jopo la majaji Monica Muganyi, Audax Ngiye na Charles Nyachae, ilikubali pingamizi la awali la walalamikiwa watatu ikiwamo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Mapema mwaka 2016, kesi hiyo ilifunguliwa na Rashid Salum Idiy na wenzake 39,999, dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Wakili Mkuu wa Serikali, Gabliel Malata, alisema mahakama hiyo ilitupilia mbali kesi hiyo katika hatua za awali kutokana na kukubaliana na hoja za mapingamizi ya awali zilizowasilishwa na mawakili wa serikali.

Malata alisema kesi hiyo ilifunguliwa mwaka 2016 na Wazanzibar 40,000, lakini walalamikiwa waliwasilisha pingamizi la awali na lililotolewa uamuzi juzi.

Katika uamuzi huo, alisema Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ilikubaliana na hoja zote za jopo la mawakili wa serikali kuhusu kutokuwa na uhalali wa kisheria wa kusikiliza shauri hilo.

Alizitaja hoja hizo ni kwamba, mahakama hiyo haina mamlaka kisheria kuhoji uwapo wa taifa huru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutoa tafsiri ya uamuzi wa nchi mbili huru zilizounda Jamhuri hiyo, ambazo kwa mujibu wa Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanganyika na Zanzibar si nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Hoja nyingine ni kwamba, wadai (Rashid Salum Idiy na wenzake 39,999), hawana hoja yoyote dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ndiyo mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa wameshindwa kuthibitisha madai yao kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, wakati hati ya Muungano wa nchi hizo mbili zinasajiliwa katika Umoja wa Mataifa na kutambuliwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna mapingamizi yaliyowasilishwa kupinga hati za Muungano kutoka kwa Tanganyika au Zanzibar.

Malata alisema mahakama pia, ilikubaliana na hoja kuwa madai ya wadai, yaliwasilishwa mahakamani nje ya muda, ambao ni siku 60 zilizotajwa katika ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pia, mahakama iliamua kila upande ubebe gharama zake kwa kuzingatia kuwa shauri hilo, liliwasilishwa kwa kuzingatia maslahi ya umma.

## Daktari atoa mbinu kuepa maradhi moyo

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAINIKA magonjwa ya moyo yanaweza kuzuilika iwapo jamii itabadili mfumo wa maisha, kwa kufuata lishe bora na kufanya mazoezi.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza, Dk. William Mahalu, aliyasema hayo juzi katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni nchini.

Dk. Mahalu aliyasema hayo akielezea kuhusu magonjwa ya moyo ikiwa ni sehemu ta maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani, ambayo hufanyika Septemba 29, kila mwaka.

Alisema kuna nchi, ambazo zimebadili mfumo wa maisha na kufuata taratibu na kupunguza idadi ya wagonjwa wa moyo, ingawa kwa hapa nchini bado ni tatizo.

"Kuna magonjwa ya moyo ya aina mbili, yale ya kuzaliwa nayo na ambayo yanakuja baada ya kuzaliwa kutokana na mfumo wa maisha. Utaratibu ambao hauzingatii mazoezi, ulaji wa nyama, mafuta na chumvi kupindukia, unasababisha magonjwa hayo," alisema.

Dk. Mahalu alisema, kila mwaka duniani watu milioni 17 hufariki dunia na kusababisha mwaka 1999, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilianzisha siku maalumu, ili jamii kutambua kuwa magonjwa hayo yanazulilika.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Samuel Rweyemamu, alisema ugonjwa wa mafindofindo (tonsils) kwa watoto walio chini ya miaka mitano umekuwa sababu ya magonjwa ya moyo kwa watoto wanaofika katika taasisi hiyo.

"Magonjwa ya virusi, bakteria huweza kusababisha moyo kutanuka. Kila siku tunaona takribani wagonjwa 200 kwa siku, idadi inaongezeka sababu tunapokea hata wagonjwa kutoka nje ya Tanzania.

Wagonjwa 1,000 tuliowachunguza baadhi walikuwa na mishipa iliyoziba kwenye moyo. Asilimia 60 hadi 70 ya wagonjwa tunawaona JKCI, wanakuwa na magojwa ya shinikizo la damu," alisema.

Dk. Rweyemamu alisema mishipa ya moyo inapopata hitilafu au kuziba katika moyo, husababisha mfumo wa umeme kwenda tofauti na kwamba hali hiyo hutibiwa kwa matibabu au kwa kuwekewa betri kwenye moyo.

Inakadiriwa asilimia 31 ya vifo vyote duniani hutokana na magonjwa ya moyo, huku wanaougua wakiwa ni watoto, watu wazima na wazee.

# Watuhumiwa mauaji kada CCM kupelekwa kortini

**Na Waandishi Wetu**

OFISI ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (DPP), inatarajia kuwafikisha mahakamani watu wanne wanaotuhumiwa kwa mauaji ya Emmanuel Polycup Mlelwa, mkazi wa Njombe.

Mlelwa alikuwa mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Vyuo Vikuu, Mkoa wa Iringa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na DPP, Biswalo Mganga, watuhumiwa hao ni Thadei Mwanyika, George Sanga, Optatus Nkwera na Goodluck Mfuse wote wa mkoani Njombe.

Kwa mujibu wa DPP, hatua hiyo ni baada ya kupitia jalada la upelelezi la watuhumiwa na kujiridhisha.

"Mnamo 21 Septemba, 2020 saa 9.30 jioni, mwili wa marehemu ambaye kwa wakati huo haukutambuliwa ulikutwa katika maeneo ya bwawa la Kibena Estate katika daraja la Mtege Kata ya Ramadhani Wilaya na Mkoa wa Njombe," ilieleza taarifa hiyo ya DPP.

"Taarifa za tukio hilo zilifikishwa katika Kituo cha Polisi cha Njombe, na hatua za kuhifadhi mwili huo hospitalini zilifanyika.

Uchunguzi wa chanzo cha kifo ulifanyika na daktari alibainisha chanzo ni ukosefu wa hewa."

"Jeshi la Polisi lilifanya upelelezi wa tukio hilo na kuwakamata watuhumiwa wanne ambao ni Thadei Mwanyika, George Sanga, Optatus Nkwera na Goodluck Mfuse."

Alisema baada ya upelelezi wa awali wa shauri hilo kukamilika, Jeshi la Polisi liliwasilisha jalada katika ofisi ya DPP kwa ajili ya kulisoma na kufanya uamuzi juu ya uwapo au la wa ushahidi unaokidhi kufungua mashtaka dhidi ya watuhumiwa kwa mujibu wa sheria.

"Nimepitia kwa makini ushahidi niliourejea kwa ufupi hapo juu na kujiridhisha kuwa unatosha kufungua mashtaka dhidi ya watuhumiwa tajwa," alisema DPP.

"Baada ya kuzingatia misingi iliyoainishwa katika Ibara ya 59B(4)(a) hadi (c) ya Katiba pamoja na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka namba 28 ya mwaka 2008."

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Frank Maxmillian, TUDARCo**



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe (katikati), akikata utepe kuzindua uwakala mpya wa magari ya Leyland Ashok na Kifaru Motors, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo na Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Afra Mbogoni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HELSB yaongeza tena muda maombi mikopo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza kuongeza siku tano kwa waombaji wa mikopo ya elimu ya juu kuanzia leo.

Taarifa ya bodi hiyo iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari, ilieleza kuwa nyongeza hiyo ya muda inalenga kutoa muda kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) hivi karibuni ili kuomba mikopo kwa njia ya mtandao ambao utafunguliwa kwa siku tano.

Taarifa hiyo ilibainisha kwamba unatokana na maombi ya wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi wahitaji ambao hawakuomba au kukamilisha maombi yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kujiunga na mafunzo katika kambi mbalimbali za JKT kwa mujibu wa sheria.

Aidha, katika muda huo wa siku tano, mfumo pia utakuwa wazi ili kuwawezesha waombaji ambao maombi yao yana upungufu kurekebisha kwa kuweka nyaraka sahihi ili kuiwezesha HESLB kuendelea na hatua nyingine.

"Kwa wanaorekebisha taarifa, wanapaswa kuingia katika akaunti zao walizofungua kuombea mkopo na watapata ujumbe kuhusu maeneo ya kurekebisha.

"Tunawasihi watumie muda huu wa siku tano kurekebisha na kukamilisha maombi yao ili kutuwezesha kuendelea na hatua inayofuata ili hatimaye wenye sifa wawezeshwe kutimiza ndoto zao," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru.

Katika mwaka wa masomo 2020/2021, serikali imetenga Sh. bilioni 464 zitakazowanufaisha wanafunzi 145,000.

Kati yao, wanafunzi 54,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza na wengine 91,000 ni wanafunzi wanufaika wanaoendelea na masomo.

Kwa mwaka wa masomo wa 2019/20 Sh. bilioni 450 zilitengwa na kuwanufaisha wanafunzi 132,119.

# Maofisa utumishi serikalini waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itasimamisha mishahara ya maofisa utumishi watakaozembea na kusababisha watumishi wa umma nchini kutolipwa mishahara yao kwa wakati.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Francis Michael, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya wiki mbili ya mfumo mpya wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa kundi la pili la maofisa utumishi na maofisa tawala 140, jijini hapa.

Maofisa hao ni kutoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Kigoma na Tabora.

Dk. Michael alisema serikali itasimamisha mishahara hadi hapo watakapohakikisha watumishi hao wamelipwa mishahara yao.

Alisema kuna tatizo katika baadhi ya taasisi za umma ambapo maofisa utumishi wanajifanya miungu watu wakati wajibu wao ni kumtengenezea mazingira mazuri ya kikazi mtumishi ili ajisikie yuko sehemu salama na kutekeleza majukumu yake.

"Msiwafanye watumishi mnaowasimamia kuona sehemu ya kazi kama jehanamu. Mbadilike kwani serikali haitamvumilia yeyote atakayekinzana na azma yake ya kuboresha huduma kwa wananchi," alisema Dk. Michael.

Aliwataka maofisa utumishi kubadilika kwa kuwajengea mazingira watumishi wa umma kuipenda serikali yao kwa sababu inawajali na kuthamini mchango wao katika maendeleo ya taifa.

Dk. Michael alisema serikali inamhakikishia mtumishi usalama wa ajira yake tofauti na sekta binafsi, hivyo hakuna ofisa utumishi atakayevumiliwa pindi akisababisha serikali kulaumiwa na watumishi wa umma au wananchi.

Naye Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Boniface Chatila, kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo, aliahidi kuwa, wakirejea katika maeneo yao ya kazi watahakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu ili kuondoa kero ya watumishi wa umma kufuata huduma Ofisi ya Rais Utumishi Dodoma.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu serikalini, ACP Ibrahim Mahumi, alisema suala la mtumishi kukosa mshahara hivi sasa linachukuliwa kama ni kosa kubwa hivyo ofisa utumishi atakayebainika atasimamishiwa mshahara ikiwa ni hatua ya awali na atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mfumo huo mpya utaanza kutumika rasmi Novemba, mwaka huu, baada ya kukamilika kwa mafunzo ya makundi yote ya maofisa utumishi na maofisa tawala ambao ndio wenye jukumu la kuutumia mfumo huo kiutendaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uandishi habari wenye weledi utaliponya taifa

**MWISHONI** mwa wiki wakati wa hafla ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari jijini Tanga, Mkuu wa Mkoa huo, Martin Shigela, alivipongeza vyombo vya habari nchini kwa kuripoti uchaguzi bila upendeleo.

Alisema ukisoma magazeti au kuangalia kituo cha radio au luninga utakuta habari ya mgombea mmoja pekee bali wote pamoja na sera za vyama vingine jambo ambalo linawasaidia wananchi kufanya maamuzi sahihi.

Alisema kupitia vyombo vya habari vinavyotoa habari bila upendeleo, vimeendelea kufanya taifa kuwa na umoja ni kuliponya na kulisaidia. Kiongozi huyo alisema kama kungekuwa na vyombo vya habari vinavyochochea, kufitinisha taifa lisingekuwa na umoja.

Pongezi hizi ni muhimu sana na zina ujumbe mzito kwa vyombo vya habari kuhakikisha vinatenda haki katika kuripoti habari za uchaguzi, kujiepusha na habari ambazo kwa namna yoyote zinaligawa taifa vipande vipande.

Pia, kutambua kuwa watu wanafuatilia utendaji kazi wa vyombo na wana nafasi ya kuvihukumu kwa namna nyingi baada ya uchaguzi, pia vitambue kuna maisha baada ya uchaguzi, wajibu wao katika jamii na watu wanaishi kwa kutegemeana.

Wakati sifa hizo zinatolewa, vipo baadhi ya vyombo vya habari vimeingia kwenye mtego wa wanasiasa wa kuchafua wengine, jambo ambalo ni baya kwa kuwa chuki ikihubiriwa mara kwa mara itajaa kwenye vifuo vya wahusika na wafuasi wao ambao wanaweza kuchukua hatua. Upo ushahidi wa baadhi ya nchi zilivyoingia kwenye machafuko ambayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na vyombo vya habari, mathalani mwaka 1994 Rwanda iliingia katika mauaji ya kimbari na kusababisha mamia ya watu kufariki na wengine wakijeruhiwa.

Kwa kiasi kikubwa vyombo vya habari vilichangia kuhubiri ukabila na chuki dhidi ya kundi jingine kiasi cha kufikisha watu kuchukiana na kuingia kwenye kulipiziana visasi.

Mfano mwingine ni uchaguzi wa Kenya mwaka 2008 ambao ulisababisha mamia ya watu kuuawa, kujeruhiwa na wengine kupoteza makazi, na yote ilichangiwa na baadhi ya vyombo vya habari kuhubiri na kuchochea chuki.


Katika nadharia ya kuitambua jamii na uwezo wake wa kuchambua mambo na kufikia uamuzi fulani, tunaeelezwa jamii ya sasa ni yenye mchanganyiko wa watu walioelimika na wasioelimika, wakiwamo ambao hawatafiti mara mbili kabla ya kufanya maamuzi.

Kwa muktadha huo, jamii hiyo inaweza kuchukua maamuzi dhidi ya kile kilichoandikwa au kutangazwa na redio au luninga na mwisho kusababisha madhara makubwa ambayo yatakuwa ni majuto. RC amtoa sifa hizo ambazo zinachagiza vyombo vya habari kufanya vizuri zaidi kwamba wakati huu siyo wa baadhi ya vyombo vya habari kuhubiri chuki, kuumiza wengine kwa kupendelea wengine au kutumia kalamu zao vibaya.

Iwapo mwanasiasa watataka kutumia chombo cha habari au mwanahabari kwa maslahi yake binafsi ya kisiasa, ni lazima kumtambua na kutompa nafasi, kwa kuwa kuendelea kuhubiri chuki na ubaguzi ni kuiharibu jamii ambayo siku ikichukua maamuzi ni sawa na mlipuko wa bomu. Katika kipindi hiki cha uchaguzi ndicho nchi nyingi huingia kwenye machafuko na kutokuelewana. Kimsingi, majeraha ya uchaguzi yanaweza kudumu kizazi hadi kizazi hivyo madhara yake yanaweza kuirudisha nchi nyuma kimaendeleo kiasi kwamba kila kilichofanyika kikawa sifuri.

Kalamu ni nzuri sana kwa kuwa humjenga au kumbomoa mtu kwa haraka sana, pia huchonganisha na kuifanya jamii kuchukua maamuzi magumu. Kutokana na matokeo mabaya ya uandishi wa habari wa uchonganishi, wanasiasa wanapaswa kuchunga ndimi zao na matendo yao katika kusaka madaraka. Wahakikishe amani inahubiriwa kwa malengo mema. Isiwe kinyume chake huku nyuma ya pazia wanatumia upanga kuangamiza wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mbio safari kuelekea uchaguzi mkuu, yafaa haya kuzingatiwa

Na Ester Mgidula, UDSM

**SASA** zinahesabika siku 27 au wiki kadhaa tu kufikia Oktoba 28, kukamilika siku iliyotarajiwa, kila Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea na amejiandikisha, uwanja ni wake kuwachagua viongozi wapya; rais, wabunge na madiwani.

Matokeo yake yanatarajiwa kufungua kazi ya kupokezana vijiti vya uongozi na wengine kuviendeleza kwa miaka mitano ijayo. Ikumbukwe, uchaguzi huo utakuwa ni wa sita tangu kuasisiwa kwa demokrasia ya vyama vingi nchini mwaka 1992, baada ya kuwapo mfumo kama huo awali kabla ya mwaka 1964.

Kwa sasa, wagombea wanaendelea kuzunguka kwenye majimbo mbalimbali kufanya kampeni zao, wakitoa ahadi mbalimbali watakazozitekeleza baada ya kuchaguliwa na wananchi.

Wakati hayo yanaendelea, tujikumbushe mambo kadhaa ya kuzingatiwa, ili uchaguzi uwe wa amani, haki na huru. Mosi, ni kudhibiti vitendo vyote vya rushwa. Kumekuwapo wimbi kubwa la tuhuma za vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi, ambapo wagombea hutoa hongo ya pesa taslimu, kofia, khanga, mashati, vinywaji na vyakula kwa lengo la kuwashawishi wapigakura.

Wagombea na wapigakura wanapaswa kujua kuwa, moja kati ya madhara makubwa yatokanayo na rushwa wakati wa uchaguzi, ni kurudiwa kwa uchaguzi au kuibuka vurugu zitakazoweza kuathiri amani ya nchi.

Kwa hiyo, ili kuziba mianya yote ya rushwa inayojitokeza, ni busara mambo kadhaa yakatekelezwa:

Kutolewa elimu inayohusu haki na wajibu wa mpigakura katika mchakato mzima wa uchaguzi, kuimarisha vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria na taratibu za uchaguzi, zikiwamo mahakama na vyombo vya usalama.

Aidha, kuna suala la haja ya kuwekwa mikakati itakayowabana wanasiasa wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Lingine, ni vita vya kukabili matabaka, sambamba na dalili zozote za kuwapo matabaka, ambayo huwa yanazaa ubaguzi, wagombea na wapigakura wanajikuta wamezama kwenye dimbwi hilo la kubaguana, sababu tu ni uwapo wa tofauti za vyama, kidini na kikabila.

> **Kutolewa elimu inayohusu haki na wajibu wa mpigakura katika mchakato mzima wa uchaguzi, kuimarisha vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria na taratibu za uchaguzi, zikiwamo mahakama na vyombo vya usalama.**

Hali ilivyo sasa kwa wananchi, kuna baadhi wanajiona ni bora kuliko wengine, kwa sababu tu ya kuwapo kwenye chama fulani chenye nguvu kuliko kingine, jambo linaloweza kuibua vurugu.

Maana yake nini? Watanzania wanatakiwa kujua kuwa 'maendeleo hayana chama' kauli ambayo mara nyingi imekuwa ikitolewa na Rais Dk. John Magufuli. Pia, hata matabaka ya kidini yanayoenda kinyume kuanza kuegemea upande ndani ya uchaguzi, yanapaswa kudhibitiwa.

Kuna wakati kulishuhudiwa madai, baadhi ya viongozi wa kidini wanaofikia hatua ya kutenga muda wa kuwashawishi waumini wao kuegemea pazuri. Historia zipo katika siasa, kujengeka matabaka ya kikabila, hayo nayo yanapaswa kuondolewa, kwani kuna maeneo ambayo wapigakura hutaka kuwapata viongozi kutoka kwenye makabila yao.

Vitendo vya namna hiyo ni hatari, kwani vinaumba utabaka unaoweza kuufanya uchaguzi kutokuwa wa haki, huru na amani.

Mwisho, ni udhibiti matumizi ya lugha isiyofaa. Ni muhimu, kwani kampeni za kistaarabu ndio jambo muhimu.

Haipendezi na hairuhusiwi kwa mgombea kumchafua mgombea mwingine kwenye kampeni kwa kutumia lugha za kejeli, matusi na vitisho, zinazoweza kuibua migogoro baina yao. Hivyo, ifikapo Jumatano ya Oktoba 28 mwaka huu, Watanzania wote wenye sifa za kupiga kura, tusiache kufika kwenye vituo vyetu vya kupigia kura kuchagua tunaowakubali, kwa njia ya amani.

**Alamsiki.**

MAKALA

# China daima inasimamia muunganiko wa nchi nyingi

MWAKA huu ni maadhimisho ya miaka 75 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa (UN). Miaka 75 iliyopita imeshuhudia maendeleo makubwa katika jamii ya wanadamu, mabadiliko makubwa katika hali ya kimataifa, na maendeleo ya haraka ya pande nyingi.

Jumuiya ya kimataifa imepata majaribio mengi na kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko makubwa ambayo hayaonekani katika karne moja. Janga la COVID-19, ambalo limeenea ulimwenguni, limeuweka ulimwengu katika njia panda kwa kasi ya haraka.

Nchi ulimwenguni zinashirikishana masilahi yaliyofungamana zaidi na maisha yao ya baadaye yakiunganishwa kwa karibu zaidi kuliko hapo awali.

Sababu ya amani na maendeleo ulimwenguni imekumbana na majaribu yasiyokuwa ya kawaida na shida nyingi.

Mshikamano au kuvunjika, ushirikiano au makabiliano, kushirikishana matatizo au kulaumiana? Wanadamu wanapaswa kufanya uchaguzi muhimu katika njia panda hii.

Ni kutokana na hali hii ya nyuma ndipo Mkutano Mkuu wa 75 wa UN ulifanyika.

Rais Xi Jinping wa China alihudhuria Mkutano wa Mkuu wa Kuadhimisha Miaka 75 ya UN, Mjadala Mkuu wa Mkutano wa 75 wa Baraza Kuu la UN na alikutana na Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres kupitia mtandao.

Katika mikutano hii, Rais Xi, akiwa wa maoni ya kimkakati ya muda mrefu na kutokana na mtizamo mpana wa kihistoria, alijibu maswali kadhaa muhimu: Je! Wanadamu wanakabiliwa na ulimwengu wa aina gani? Ni aina gani ya UN inahitajika kwa ulimwengu? Je! Ulimwengu unakumbana na China ya aina gani?

Ni wakati tu tunapojua ni aina gani ya ulimwengu unaokabili wanadamu tunaweza kwenda thabiti na mbali kwenye njia inayofaa. Janga la COVID-19 ni kama kioo.

Haionyeshi tu ugumu katika maendeleo ya ulimwengu, lakini imeonyesha shida zinazoendelea katika muundo wa maendeleo ya binadamu na mtindo wa maisha, na viungo dhaifu katika mfumo wa utawala wa ulimwengu. Kwa muhtasari "mafunzo manne" yaliyoletwa na COVID-19 kwa wanadamu, Rais Xi alielezea wazi mwenendo wa nyakati.

COVID-19 inatukumbusha kuwa tunaishi kijiji kilichounganishwa cha ulimwengu na mtizamo mmoja, na kwamba kufuata sera ya mwombaji-jirani yako au tu kuangalia kutoka mbali wakati wengine wako hatarini mwishowe itatupelekea kwenye shida ile ile inayokabiliwa na wengine. Kwa hivyo, lazima tukatae majaribio ya kujenga ukanda kuwaacha wengine nje na kupinga kunufaika kwa upande mmoja huku mwingine ukipoteza.

Lazima tukumbatie maono ya jamii yenye mustakabali wa pamoja ambao kila mtu ameunganishwa pamoja.

Lazima tuonane kama washiriki wa familia moja kubwa na tufuate ushirikiano wenye faida kwa wote. Utandawazi wa kiuchumi ni uhalisia usiopingika na ni mwenendo wa kihistoria.

Ulimwengu hautawezi kurudi kujitenga. Hakuna mtu anayeweza kukata uhusiano kati ya nchi na nchi.

Lazima tukabiliane na maswala hayo makuu kama pengo la utajiri na mgawanyiko wa maendeleo. Lazima tufuate maendeleo ya wazi na jumuishi, tuendelee kujitolea kujenga uchumi wazi wa ulimwengu, na kusema "hapana" kujinufaisha kwa upande mmoja na kujihami.

Njia iliyopigwa ya kuchimba rasilimali bila kuwekeza katika uhifadhi, kufuata maendeleo kwa gharama ya kujihami, na kutumia rasilimali bila urejeshwaji sio endelevu.

Binadamu anapaswa kuzindua mapinduzi ya kijani na asonge haraka kuunda njia ya kijani ya maendeleo na maisha. Tunapaswa kufanya juhudi kufanikisha ahueni ya uchumi wa kijani wa ulimwengu katika kipindi baada ya COVID na kuunda nguvu kubwa inayoendesha maendeleo endelevu.

Mfumo wa utawala wa ulimwengu unahitaji mabadiliko na uboreshaji. Lazima tudumishe ukweli wa pande nyingi na kulinda mfumo wa kimataifa na UN kama msingi wake, tufuate kanuni ya mashauriano mapana, ushirikiano wa pamoja na faida za pamoja, na kukuza mageuzi ya mfumo wa utawala wa ulimwengu ili iweze kuendana na mabadiliko ya kisiasa na mienendo ya kiuchumi, hukutana na changamoto za ulimwengu na kukumbatia hali ya msingi ya amani, maendeleo na ushirikiano wa ushindi wa pande.

Kuhusu swali "ni aina gani ya UN inahitajika kwa ulimwengu", Rais Xi Jinping aliwasilisha "pendekezo la mawazo manne", ambalo lilijibu swali kwa njia ambayo inasimamia madhumuni ya Mkataba wa UN na kuendana na mwenendo wa kihistoria.

Tunahitaji UN ambayo inasimama imara kwa haki, inazingatia kanuni ya kuheshimiana na usawa kati ya nchi zote, kubwa au ndogo, inaendelea katika mashauriano makubwa, ushirikiano wa pamoja na faida za pamoja, na inapinga ukatili, uonevu na ukuu.

Tunahitaji UN ambayo inasimamia utawala wa sheria, inalinda bila kusita madhumuni na kanuni za Mkataba wa UN, na inaratibu uhusiano kati ya nchi na masilahi yao kulingana na sheria na kanuni. Nchi ulimwenguni hazipaswi kutawaliwa na wale wanaonyoosha ngumi kwa wengine, na haipaswi kuwa na mazoezi ya ubaguzi na upendeleo.

Tunahitaji UN ambayo inakuza ushirikiano, inachukua nafasi ya mzozo na kuleta mazungumzo, malazimisho na kuleta mashauriano na ushindi wa pande moja na kuleta ushindi wa pande zote , na inakusudia kujenga familia kubwa ya ulimwengu ya maelewano na ushirikiano.

Tunahitaji UN ambayo inazingatia hatua halisi, ikilenga utatuzi wa shida na kuelekea matokeo dhahiri kwani inaendeleza usalama, maendeleo na haki za binadamu sambamba.

Kipaumbele kinapaswa kuzingatiwa kushughulikia changamoto zisizo za jadi za usalama kama afya ya umma, na kuwe na msisitizo mkubwa juu ya kukuza na kulinda haki za kujikimu na maendeleo.

Ambayo ulimwengu unakumbana nayo", Rais Xi alitoa sauti za Wachina na akafanya ahadi za Wachina kwa kuongeza safu ya mapendekezo ya wazi ya sera na hatua za vitendo na mipango.

Kama nchi kubwa inayoendelea ulimwenguni, China inafuata njia sahihi iliyo na maendeleo ya amani, uwazi na ya ushirika. China haitawahi kutafuta mamlaka, kujipanua au nyanja za ushawishi.

Haina nia ya kupigana ama vita baridi au vita moto na nchi yoyote. Haitafuti kujiendeleza yenyewe au kushiriki kwenye mchezo wa kujinufaisha.

Badala ya kutafuta maendeleo nyuma ya milango iliyofungwa, China inalenga kukuza, kwa muda, dhana mpya ya maendeleo na mzunguko wa ndani kama msingi na mzunguko wa kimataifa wa ndani ukijiimarisha, ambayo itaongeza msukumo wa kufufua uchumi na ukuaji wa uchumi.

Kufuatia mikutano ya Mikuu ya kwa ajili ya kuadhimisha miaka 70 ya UN iliyofanyika mwaka 2015, Rais Xi Jinping, kwa mara nyingine, alitangaza "hatua nne" katika Mkutano Mkuu wa UN kuunga mkono jukumu kuu la UN katika maswala ya kimataifa.

China itatoa dola nyingine milioni 50 kwa mpango wa Umoja wa Mataifa wa Matokeo ya Binadamu (UN COVID-19 Global Human Result Plan); China itatoa Dola za Marekani milioni 50 kwa Mfuko wa Dhamana ya Ushirikiano wa Kusini-Kusini ya China-FAO (Awamu ya Tatu); China itapanua Mfuko wa Dhamana ya Amani na Maendeleo kati ya UN na China kwa miaka mitano baada ya kumalizika mwaka 2025; China itaanzisha Kituo Cha Maarifa Cha Upatikanaji wa Taarifa za Kijiografia na Ugunduzi Cha UN na Kituo Cha Utafiti Cha Kimataifa Cha Taarifa Kubwa kwa ajili ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, ili kufanikisha utekelezaji wa Agenda 2030 ya Maendeleo.

Kwa kuongezea, Rais Xi alisisitiza azimio thabiti la China katika kujihusisha kikamilifu katika mapigano ya kimataifa dhidi ya COVID-19 na kuchangia sehemu yake katika kudumisha usalama wa afya ya umma duniani.

Alisema kuwa China itaendelea kushiriki njia zake za kudhibiti magonjwa ya mlipuko na vile vile uchunguzi na tiba na nchi zingine, kuhakikisha kuzuia kikamilifu usambazaji wa magonjwa ya mlipuko, na kushiriki kikamilifu katika utafiti wa ulimwengu juu ya kutafuta chanzo na njia za usambazaji wa virusi.

Rais Xi Jinping kwa mara nyingine alisisitiza kuwa chanjo za COVID-19 zilizotengenezwa na China, mara moja zikiwa tayari kwa matumizi, zitatengenezwa kuwa faida ya umma ulimwenguni na zitapewa nchi nyingine zinazoendelea kwa msingi wa kipaumbele. Vitendo vinaongea zaidi kuliko maneno.

Katika kubeba majukumu makubwa ya nchi na kuboresha ustawi wa wanadamu, China siku zote ni nchi ya vitendo ambavyo vinalingana na maneno, mjenzi wa amani ya ulimwengu, mchangiaji kwa maendeleo ya ulimwengu na mtetezi wa utulivu wa kimataifa.

Katika njia sahihi ya kutetea ushirikiano wa pande nyingi, China haijawahi kuwa "mpweke".

Nchi nyingi duniani, pamoja na Tanzania, ni "wasafiri wenzao" wa China ambao hufanya ushirikiano wa kimataifa.

China na Tanzania daima zinaheshimu haki ya kila mmoja ya kujitegemea kuchunguza mfumo wa kisiasa na njia ya maendeleo, na kudumisha mawasiliano ya karibu na ushirikiano katika maswala ya ulimwengu kama vile mageuzi ya UN, mabadiliko ya hali ya hewa, mageuzi ya Shirika la Biashara Ulimwenguni na kupambana na magonjwa ya mlipuko.

China na Tanzania zimejitolea kulinda maslahi ya pamoja ya nchi zinazoendelea na kukuza utaratibu wa usawa na wa kuridhisha zaidi wa kimataifa.

Mbeleni, China itafanya kazi na nchi nyingine zenye urafiki kote ulimwenguni kudumisha ujamaa na kulinda mfumo wa ushirikiano wa pande nyingi, kudumisha amani na kukuza maendeleo ili kuunda mustakabali mzuri wa ulimwengu.


Mhe. Wang Ke, Balozi wa China nchini Tanzania

# Msimamo wa JPM kuhusu corona wawanufaisha wafanyabiashara

**Na Beatrice Moses,** TUDARCO

MSIMAMO wa Rais John Magufuli wa kutozuia shughuli za kijamii wakati wa ugonjwa wa corona, umetajwa kunufaisha baadhi ya wafanyabiashara na benki kuendelea kutoa huduma bora zilizonufaisha wateja na jamii kwa ujumla.

Akizungumza jana kwenye kongamano la kibiashara lililoandaliwa na Benki ya NMB na kukutanisha baadhi ya wafanyabiashara wakubwa na wa kati kutoka maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Biashara wa benki hiyo, Alex Mgini, alisema corona ilizua changamoto kwenye maeneo mengi yakiwamo ya kibiashara.

Mgini alisema uwapo wa corona nchini, ulisababisha hofu miongoni mwa jami na mdororo wa biashara katika maeneo mengi. Kutokana na hali hiyo, mwongozo ulitolewa na wataalamu wa afya ikiwamo kuhamasisha kujitenga (social distance) na pia kutumia vifaa vya kuzuia kuenea kwa virusi vya Covid- 19, vinavyosababisha ugonjwa wa corona.

"Kauli ya uhamasishaji wa kufanya kazi kwa bidii katika kipindi hicho iliyotolewa na Rais Magufuli ilikuwa chachu katika maeneo ya kazi. Pengine watu wangekufa na njaa badala ya corona. NMB tulijipanga, baadhi ya wafanyakazi walitakiwa kufanyia kazi nyumbani, wengine ofisini, hivyo hatukutetereka katika kutoa huduma," alisema Mgini.

Alisema NMB iliandaa mipango mbalimbali ya kuwasaidia wafanyabiashara chini ya mwongozo uliotolewa na Benki Kuu (BoT) kwa kuwasikiliza wafanyabiashara walioyumba kutokana na corona.

Katika kuitikia hilo, alisema benki iliwaongezea wafanyabiashara muda wa kurejesha mikopo na wengine kupunguza riba.

Mwenyekiti wa Klabu ya Wafanyabiashara NMB, Award Mpandila, alisema hatua iliyochukuliwa na benki hiyo kuwaongezea muda wa marejesho, umewasaidia kusimama tena kibiashara.

"Ni wazi wako ambao wangefilisika, lakini kwa sababu benki ilielewa tulipowaeleza athari zilizotukabiri, tumesimama tena na kusonga mbele," alisema Mpandila.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha NMB, Benedictor Baragomwa, ambaye ni mlezi wa klabu hiyo, alisema kuwa benki ipo vizuri




Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts (wa tatu kushoto), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa mpango wa uwezeshaji kwa wastaafu uliyofanyika jijini Dar es Salaam, jana. Wengine ni Mwenyekiti wa makatibu Wakuu Wastaafu, Michael Mwanda, Balozi Mstaafu Salome Sijaona, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati Benki hiyo, Boma Raballa, Mwenyekiti wa Umoja wa Polisi Wastaafu, Suleiman Kova na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya CRDB, Adili Stephen. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BRELA yatoa elimu usajili biashara

**Na Christina Njovu,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amewataka maofisa biashara nchini kuwa wasaidizi na washauri wa wafanyabiashara na wawekezaji, ili kuwa chachu ya uwekezaji, ukuaji na uanzishwaji wa biashara.

Alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya utoaji wa huduma za sajili na leseni kwa njia ya mtandao kwa maofisa TEHAMA na maofisa biashara wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikiwamo mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma, yanayoendeshwa na Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA).

"Ipo kasumba iliyozoeleka kuhusu utendaji wa maofisa biashara kuwa jukumu lao kuu kwa sasa ni kama wakusanya mapato hasa sehemu za biashara, vilabuni na kwenye nyumba za kulala wageni, badala ya kuwa wasaidizi na washauri wa wafanyabiashara na wawekezaji," alisema Andengenye. Alisema anatarajia kuwa mafunzo hayo yatasaidia kubadili fikra na mitizamo ya maofisa biashara na watendaji wengine wa serikali kuwa watoa huduma na msaada kwa wafanyabiashara, hivyo ni vyema wakafuatilia mafunzo hayo vizuri, ili watakaporudi katika vituo vyao vya kazi watumike kama chaji ya uwekezaji, ukuaji na uanzishwaji wa biashara.

Andengenye alisema, maofisa biashara wanatakiwa kubadili fikra na kutakiwa kuwa kimbilio la watu wanaotaka kuanzisha biashara na wafanyabiashara wajivunie uwapo wao.

Mafunzo hayo yana lengo la kuwawezesha wataalamu wa TEHAMA na biashara kwenda kuwahudumia wananchi katika maeneo yao kwa wepesi na weledi kwa kuwa mlolongo mrefu uliwakatisha wafanyabishara wengi tamaa na kushindwa kusajili.

Aliwataka washiriki wawe chachu ya kusambaza elimu kwa wananchi na nyenzo ya kupunguza kero mbalimbali na gharama ya urasimishaji biashara suala, ambalo mara kwa mara serikali imekuwa ikilipigia kelele.

Naye Ofisa Tawala na Rasilimali Watu Mkuu wa BRELA, Migisha Kahangwa, alisema kuwa BRELA inaendesha mafunzo hayo kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi, kitendo cha kuwajengea uwezo maofisa biashara hao kutawezesha wafanyabiashara kupata msaada wa karibu katika kurasimisha biashara zao badala ya kuifuata BRELA, Dar es Salaam.

# Sumaye: Watanzania wasifanye makosa

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI Mkuu mstaafu wa awamu ya tatu, Frederick Sumaye, amewataka Watanzania kutofanya makosa katika kuchagua Rais kwa sababu suala la kuongoza nchi siyo sawa na kucheza kamari.

Akizungumza jana katika mkutano wa kampeni uliofanyika mjini Katesh Jimbo la Hanang' ambao uliandaliwa kwa ajili ya mgombe mwenza wa CCM, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alisema wananchi wahakikishe wanamchagua rais ambaye atawaletea maendeleo.

"Msifanye mambo ya kubahatisha kuongoza nchi siyo kamari, kamari unaweza kula (kushinda) hata kama hupangilii inategemea tu lile dude limelala upande gani," alisema.

Sumaye alisema hali ya upinzani bado kupewa nafasi ya kuongoza nchi kwa sababu baadhi havijajipanga hata katika mfumo wao wa uongozi," alisema.

"Sasa nyie watu wa Hanang' mimi ni mzee wenu, nimerudi CCM msije mkaniabisha mkapiga kura CHADEMA, ACT sijui nani hao bado kabisa," alisema, Sumaye ambaye, aliwahi kuwa kada wa CHADEMA kabla ya kurejea CCM hivi karibuni.

Alisema Rais John Magufuli, ambaye ni mgombea wa CCM amesaidia sana kuinyoosha nchi na sasa inakwenda katika mstari unaoelewe-ka.

Aliongeza kuwa hivi sasa ukienda ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mtendaji wa Kata ambao zamani walikuwa wakiitwa Mungu watu na wakurugenzi wa halmaashauri hivi sasa unapewa huduma sana.

"Tuliomba Rais anayesimamia nidhamu anayepambana na ufisadi sasa leo tunamuona Rais Magufuli hafai, kweli?" alihoji.

Sumaye alisema baadhi ya wenyeviti na makatibu wakuu wa vyama vya siasa hawako na wagombea urais wa vyama vyao.



Mwezeshaji wa semina kwa walezi wa klabu za jinsia katika shule za msingi na sekondari na vituo vya taarifa na maarifa, Beatrice Ezekiel, akiendesha semina hiyo, iliyoandaliwa na Jukwaa la Vijana Wanaharakati (YFF), kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sekta binafsi yapewa somo kukabili athari za tabianchi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI imezitaka sekta binafsi kutambua sera za nchi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuondoa changamoto zinazoikabili.

Imeelezwa kuwa changamoto hizo kwa kiasi kikubwa zinatajwa kuathiri sekta ya kilimo.

Akizungumza katika kongamano la kitaifa wadau la jukwaa la kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi, mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Hadija Kayera, alisema kutofautiana huko kisera kumechangia kutokuwa na mwelekeo mmoja wa kukabiliana na atahari hizo.

Alisema serikali imeweka sera katika masuala ya kilimo, ardhi na misitu ambazo zimeonyesha mafanikio katika kusaidia wakulima kukabiliana na mabadiliko hayo.

"Kujua sera za nchi zinataka nini ndio itasaidia kuzifanyia kazi kwa pamoja ili isije kutokea sekta binafsi zinafanya kivyake na serikali ina sera zake...inafika mahali hatuendi sawa na wakulima wetu nchini, wanaendelea kusumbuliwa na mabadiliko ya tabianchi," alisema Kayera.

Obedia Nyagiro, mkurugenzi wa sera na mipango Wizara ya Kilimo, alisema miongoni mwa sera zinazotekelezwa na serikali katika kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na kuanzishwa kwa skimu za umwagiliaji.

Alisema katika kutekeleza sera, zaidi ya skimu za umwagiliaji 179 zimejengwa katika kipindi cha miaka 5 tangu mwaka 2016 hadi 2020 katika maeneo mbalimbali nchini ambapo zimeanza kuonyesha matunda.

"Tumejenga skimu 179 nchi nzima tangu serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani kati ya hizo zipo 16 ambazo ni kubwa na nyingine zinaendelea kuhudumia wakulima wadogo wadogo, hii ni kwa sababu tunataka wakulima wetu walime kwa tija bila kutegemea mvua mabazo zimekuwa changamoto kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema Nyagiro.

Naye mwenyekiti wa jukwaa la wadau wa kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi (TCSAA), Stephano Kingazi, alisema teknolojia zilizogunduliwa na wataalamu zinatakiwa kutumiwa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. "Kama nchi hatuwezi kujitenga na sayansi na teknolojia kwa sababu ya kukua kwake na kimsingi mabadiliko ya tabia ya nchi bado ni changamoto kwa wakulima wetu hivyo ipo haja kwa serikali kufanya maboresho katika sera za sekta ya kilimo na ardhi ili tuweze kutumia vizuri teknolojia za wataalamu zilizoletwa," alisema Kigazi.

# Swissport yaipa neno serikali corona

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya kuhudumia mashirika ya ndege, abiria na mizigo (Swissport), imesema hatua zilizochukuliwa na serikali katika kudhibiti ugonjwa wa corona ikiwamo kuruhusu safari za ndege za ndani na nje, zimeanza kuzaa matunda.

Imesema biashara imerudi katika hali yake ya awali baada ya kuyumba kwa kipindi kifupi cha uwapo wa ugonjwa huo nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa Swissport, Mrisho Yassin, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana ikiwa ni kumbukumbu ya shirika hilo kutimiza miaka 35 ya utoaji huduma hiyo nchini.

Yassin alisema kabla ya kuingia nchini ugonjwa wa corona, walikuwa wanafanya biashara na kuingiza faida kubwa, lakini baada ya ujio wa ugonjwa huo na baadhi ya mashirika ya ndege kusitisha huduma zake, walipata hasara ya Sh. bilioni 1.2 kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu.

"Hatua zilizochukuliwa na serikali kupambana na COVID-19, kibiashara zimesaidia kwa kiwango kikubwa na biashara zimeanza kurudi katika hali yake ya kawaida,"alisema Yassin.

"Tunazungumzia hali ya biashara kurudi kwa sasa kwa sababu hofu ya ugonjwa huo kwa nchi yetu siyo kubwa kulingana na namna serikali yetu ilivyoudhibiti na ndiyo maana mashirika mengi yamekuwa na imani ya kuja Tanzania bila kuhofia na jambo lolote . Nipongeze juhudi hizi kwa sababu zimetusaidia."

Alisema mpaka sasa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ndilo limeendelea kuongoza kwa kurusha ndege zake nyingi kupitia kampuni hiyo tofauti na ilivyo kwa zile zinazotoka katika mashirika mengine.

Alisema kabla ya kuingia ugonjwa huo wa corona, ndege za shirika hilo zilizokuwa zikiruka kwa siku ni 35 na baada ya ujio wa ugonjwa huo zilipungua.

Alisema tayari zimeanza kurudi tena katika hali yake ya kawaida na kwamba mpaka sasa ndege kutoka shirika hilo zinazoruka kila siku ni zaidi ya 20.

# Vijiji 73 Missenyi vyapata umeme

**Na Mwandishi Wetu**

VIJIJI 73 kati ya 77 vya Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera vimepelekewa huduma ya umeme. Hayo yalisemwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Kassim Majaliwa, wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Kassambya, katika mkutano uliofanyika kwenye uwanja wa Mashujaa, wilayani Missenyi.

Amevitaja vijiji ambavyo havina umeme na vipo kwenye mpango wa kupelekewa umeme ni vijiji vya Buchurago, Katano, Kakunyu na Bugango.

Akizungumzia sekta ya mifugo ambayo imetajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 hadi 2025, Majaliwa alisema serikali imeisimamia vizuri sekta ya mifugo, ili kuhakikisha wafugaji wanapata manufaa.

"Shilingi milioni 23 zimetumika kukarabati machinjio ya Bunazi hapa Misenyi, pia tumerahisisha uuzaji wa mazao ya mifugo kwa kufuta tozo kero 114 katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kuimarisha masoko ya mazao ya mifugo kwa kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo," alisema.

Alisema serikali imepanga kuanzisha vituo vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo katika mikoa 18, ambayo haina vituo, kuimarisha huduma za tiba za mifugo kwa kuhakikisha kila wilaya ina maabara, kliniki na daktari wa mifugo.

# Wakulima wapya korosho wataka stakabadhi ghalani

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

WAKULIMA wapya wa zao la korosho katika Halmashauri ya Wilaya za Mpwampwa, Kongwa na Chamwino mkoani Dodoma wameiomba Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele na Bodi ya Korosho Tanzania kuwaunganisha na mfumo wa soko la stakabadhi gharani kama walivyo wakulima wa mikoa ya kusini ili kuwa na uhakika wa masoko baada ya kuanza uzalishaji.

Wakulima hao waliwasilisha ombi hilo kwa nyakati tofauti kwenye mafunzo ya kilimo bora cha korosho yaliyofanyika katika wilaya hizo za tatu na kuendeshwa na watafiti kutoka TARI Naliendele, Bodi ya Korosho pamoja na maofisa kilimo kutoka sehemu hizo.

Mkulima wa zao hilo, Samuel Deda kutoka Mpwampwa, alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, wameanza kulima korosho na kuanza kuvuna, lakini soko kwao limekuwa tatizo na kuomba kuunganishwa na mfumo wa masoko kama wanavyofanya wakulima wa mikoa ya kusini.

Naye Jummane Hamis kutoka Mpwapwa, alisema kuwa licha ya kuhamasika kulima zao kwa wingi, lakini hawana uhakika wa kuingizwa katika soko kwa kutumia mfumo wa soko la zao hilo, hivyo kuiomba Bodi ya Korosho na watafiti kutoka TARI Naliendele kuwaunganisha na mfumo huo.

Akijibu maombi hayo, Mratibu wa korosho kutoka TARI Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema wanachotakiwa kukifanya wakulima wa wilaya hizo ni kuanzisha vyama vya msingi vya ushirika kwa kila kijiji (AMCOS) na kuanzisha chama kikuu cha ushirika ambacho kitakuwa na uwezo wa kusimamia mfumo wa uuzaji wa zao hilo kwa kutumia stakabadhi gharani kama wakulima wa mikoa ya kusini wanavyofanya.

# Mwalimu anayedaiwa kujeruhiwa na mwanafunzi atoka hospitali

**Na Mary Geofrey**

MWALIMU Majogolo Ngwalali (36) wa Shule ya Sekondari Kiagata Butiama mkoani Mara aliyejeruhiwa na mwanafunzi wa kidato cha tatu akiwa kazini, ameruhusiwa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), baada ya kupatiwa matibabu na afya yake kuimarika.

Akizungumza baada ya kuruhusiwa kutoka MOI juzi, Ngwalali aliwashukuru wahudumu wa afya wote kwa kumpa huduma bora na anaendelea vizuri.

"Kwanza ninawashukuru madaktari na wauguzi wa MOI, wamenihudumia vizuri toka siku ile ya Septemba 24 mwaka huu, nilipofika hapa saa 6:00 usiku, nawashukuru wahudumu wa kituo cha Afya Kiagata na Hospitali ya Mara, ambako nilipata huduma za awali kabla ya kuja MOI, " alisema Ngwalali.

Kadhalika, aliishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, ambayo ilihakikisha anapata huduma kwa wakati ikiwa ni pamoja na kumtafutia usafiri wa ndege kufika Dar es Salaam.

Akisimulia namna alivyojeruhiwa, Majogolo alisema alijeruhiwa na panga na mwanafunzi wa kidato cha tatu akiwa katika ukaguzi wa kawaida wa watoro na watorokaji.

"Tulikuwa tunafuatilia watorokaji na watoro ndipo mwanafunzi wa kidato cha tatu alipo nijeruhi kwa kunikata mkono kwa panga," alisema Ngwalali.

Akizungumzia afya yake baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali, alisema anaendelea vizuri tofauti na awali alikuwa na maumivu makali.

"Namshukuru Mungu naendelea vizuri hapo awali nilikuwa na maumivu makali hadi siwezi kuchezesha vidole vyangu, lakini sasa hivi vinacheza, hii inatia moyo," alisema Ngwalali.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano MOI, Patrick Mvungi, alisema Majogolo alipokelewa hospitalini hapo alipatiwa huduma ya upasuaji wa dharura siku hiyo hiyo na sasa ameruhusiwa kurudi nyumbani baada ya afya yake kuimarika. "Tumemruhusu kwenda nyumbani kwa sababu afya yake imeimarika na anaendelea vizuri atarudi baada ya wiki mbili Jumanne kwenye kliniki zetu," alisema Mvungi.

Alisema Ngwalali alifanyiwa upasuaji mkubwa wa kurekebisha mishipa katika mkono wake wa kushoto, ambao alijeruhiwa na mwanafunzi wake akiwa katika majukumu yake katika Shule ya Kiagata Butiamma mkoani Mara.




Makamu wa Rais wa GGML, Simon Shayo (kulia), akimkabidhi kadi ya gari la wagonjwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Ali Kidakwa, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Bukoli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema zahanati kupata gari la wagonjwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Rafiki Surgical Mission kutoka Australia wametoa msaada wa gari la wagonjwa lenye gharama ya Sh. milioni 32 kuhudumia wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Bukoli na maeneo jirani wilayani Geita.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya gari hilo katika Kituo cha Bukoli wilayani Geita, Makamu Rais anayeshughulikia mahusiano na maendeleo endelevu, Simon Shayo, alisema msaada wa gari hilo umetolewa kwa wakati na utasaidia kutatua changamoto za usafiri kwa wagonjwa mahututi katika kata hiyo ya Bukoli na maeneo ya jirani.

"Halmashauri ya Wilaya ya Geita iliomba msaada wa gari la wagonjwa kutoka GGML ili kuwasaidia wagonjwa katika jamii ya watu wa Bukoli ambao walikuwa na changamoto kubwa kila ilipobidi kusafirisha wagonjwa kwa ajili matibabu makubwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Geita ambayo ipo wastani wa kilomita 35 kutoka kijiji cha Bukoli.

"Ushirikiano kati yetu na Rafiki Surgical Mission ni mwitiko wa maombi hayo na umekuja muda mwafaka kwa kuwa wamekuwa pia na dhamira ya kusaidia huduma za afya mkoani Geita kwa miaka kadhaa sasa," alisema Shayo.

Kwa karibu miaka 20 sasa, mbali na kutoa msaada wa vifaa tiba, Geita Gold Mining Limited kwa kushirikiana na Rafiki Surgical Mission wameongeza wigo wa matibabu kwa watoto na watu wazima mkoani Geita ambao wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya midomo sungura na migongo wazi kwa kuwapatia matibabu ya upasuaji bure.

Shayo alifafanua kuwa GGML pia walitoa msaada katika kituo cha afya cha Bukoli mwaka 2004 kwa kujenga jengo la wagonjwa wa nje na nyumba ya watoa huduma wa afya. GGML pia imefadhili miradi mbalimbali ya afya wilayani Geita ikiwamo ukarabati wa Hospitali ya Rufani mkoani Geita na ujenzi wa vituo vipya vya afya katika vijiji vya Nyamalembo, Nyakahongola, Kasota na Kakubiro ambapo miradi yote hiyo kwa pamoja iligharimu Sh. bilioni 1.8.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Ali Kidwaka, kwa niaba ya serikali ametambua mchango wa GGML katika kutatua changamoto ya huduma za afya katika halmashauri ya wilaya na kwingineko mkoani Geita na kuwaomba washirika wengine waliopo katika Wilaya ya Geita kushirikiana na serikali kwa lengo hilo hilo.

Aidha, mwaka 2019, GGML ilichangia pia vifaa tiba vyenye gharama ya shilingi milioni 142 katika vituo vya afya vya Katoro na Bukoli.

## DC ataka wajasiriamali kupewa elimu

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, amewataka wataalamu kuanzia ngazi ya kata kwa kutoa elimu ya ujuzi walionao kwa wajasiriamali ili miradi wanayoanzisha ikawe endelevu.

Akifungua mafunzo kwa wajasiriamali Ofisa Tarafa Mkuranga anayefuatilia sera za serikali, Clement Muya, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya, alisema wataalamu kwenye kata 25 za wilaya hiyo wanatakiwa kuwa karibu na wajasiriamali ili miradi yao iwe yenye ubora.

Aliwataka wanufaika wa mkopo hiyo kufahamu wazi kwamba fedha hizo ni za wananchi ambazo zinztakiwa zilete tja na matokeo chanya.

Awali Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Halmashauri ya Wilaya hiyo, Peter Nambunga, alisema wanaendelea kutekeleza maagizo ya serikali kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa kuwakopesha wajasiriamali wanawake vijana na watu walemavu kwa kila mwaka wa fedha.

Mhandisi Mshamu Munde, alisema mikopo hiyo ambayo haina riba inalenga kutekeleza azima ya serikali kufikia uchumi wa kati kwa kuhakikisha wananchi wanajiweza kiuchumi.

## Red Cross yasaidia jamii kwa 80%

**Na Yasmine Ptotace**

IMEELEZWA kuwa, asilimia 80 ya shughuli za kijamii zinazofanywa na Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross) Tanzania ni za kujitolea.

Hayo yalisemwa na Christopher Nzera, mwamasishaji kutoka RedCross na kuuongeza: "Tupo wanachama zaidi ya 60,000 nchini, tumekuwa tukifanya kazi kwa kujitolea."

Alisema taasisi hiyo inaisaidia serikali na mamlaka za umma, na kwamba wamekuwa wakigusa kila nyanja kwa kuisaidia jamii inapokumbwa na matatizo.

Alisema wanafanya kazi kwa uhuru badala ya kuchaguliwa na mtu yeyote shughuli za kufanya.

Katibu Mkuu Red Cross Tanzania, Julias Kejo, alisema wamekuwa wakichangia kutoa huduma ya kwanza.

# ama





Ukurasa 14

**Majaribio ya chanjo corona chuo kikuu Marekani yazua wasiwasi**



Ukurasa 12

**Unywaji duni maziwa unaoelemewa na janga la wauzaji wanaochakachua**



Ukurasa 14

Nishati mbadala na madini adimu, dhidi ya uharibifu mpya mazingira

AFYA

# MASAHIBU YA KUSHANGAZA



Celine Njoki. **PICHA: MTANDAO**

CELINE Njoki(34), ni mama wa watoto watatu nchini Kenya. Ni vigumu sana kwa mtu kuweka akilini mwake mahangaiko na uchungu mwingi ambao mama huyu amepitia katika miaka yake duniani .

Usiku mmoja mwezi Juni, mwaka wa 2016 hatasahau , wakati ule mama huyu wa watoto watatu hakuwa na makazi ya kuishi , alikuwa analala mitaani, katika nyumba moja iliyokuwa mahame.

Anakumbuka usiku wa manane alivamiwa na wanaume aliowahesabu 15 wote walim'baka mmoja baada ya mwingine na kumuacha akiwa ameumizwa sehemu za siri kiasi cha kuhitaji upasuaji , alihitaji kushonwa mara kadhaa ili aweze kwenda haja zake kama kawaida .Mama huyo anasema kuwa anashuku kuwa wanaume hao walikuwa wezi , waliokuwa wametekeleza uhalifu sehemu fulani na walikuwa hapo kugawa mali ya wizi. Ndipo wakamvamia akiwa amelala.

Baada ya mkasa huo, ilibidi asaidiwe na wasamaria. Alipata matibabu pia kiakili kutokana na unyama aliyofanyiwa, kwa msaada wa rafiki alimtambulisha kwa shirika la kuwasaidia wanawake , lililompangia nyumba na kumsaidia kwa ajira .

Maisha yalionekana kurudi kama kawaida , na alihisi kuwa angeyasahau yaliomfanyikia , ila mengi yalikuwa yanamsubiri mbele.

Siku moja mnamo mwezi Desemba mwaka wa 2017 alipokuwa anatoka kazini , jioni alivamiwa tena akiwa barabarani na wanaume aliyowahesabu kuwa wasita , wote walimbaka mmoja kwa mwengine . Maumivu na nyuzi za kale zote ziliraruka kutokana na kasi ya ubakaji .

"Hawa walionibaka hawakuniibia chochote , ninashangaa kwa kuwa haikuwa usiku lakini walifaulu kunishika kwa nguvu , baada ya kumaliza walichokifanya waliniacha hapo nikiwa hoi, nilimpigia simu rafiki wangu aliyekuja kuniokoa alinipeleka hospitalini .," anakumbuka Celine .

Celine alifanyiwa upasuaji mwengine sehemu za haja kubwa kwa kuwa alikuwa ameharibiwa tena wakati wa ubakaji .

Ubakaji wa mwisho kilimtoa moyo wa kuendelea na maisha yake , kwani alianza kujiuliza ni kwanini anakuwa muathiriwa wa ubakaji kila wakati ?

Baada ya miezi minne , Aprili mwaka wa 2018 ubakaji mwengine ulimkuta

"Walivunja nyumba yangu wakati wa usiku , wanaume hao walikuwa wamevalia barakoa , lakini nadhani kuwa ni wale wale walionibaka barabarani , kwani nilizifahamu sauti zao na hata kunusa manukato waliokuwa nayo ." anakumbuka Celine

Ubakaji wa mwisho kilimtoa moyo wa kuendelea na maisha yake , kwani alianza kujiuliza ni kwanini anakuwa muathiriwa wa ubakaji kila wakati ?

Vilevile, alianza kuwa na woga wa kutembea pekee yake kwani alikuwa na wasiwasi kila mara alipokuwa anakutana na wanaume barabarani .

Celine anasema kuwa mikasa hiyo iliripotiwa katika vituo vya polisi lakini hadi sasa hakuna hata mmoja amekamatwa.

Celine Njoki alizaliwa katika mazingira ambayo ndoa kati ya wazazi wake haikudumu . Mwanadada huyu anakumbuka akiwa na miaka minne hivi mamake aliondoka na kakake aliyekuwa mdogo , tangu wakati huo Celine hakuwahi msikia wala kumuona mama yake .

Baba yake Celine alifanya kila awezalo kuwapa watoto wake mapenzi ya mama na ya baba na maisha ya kawaida Celine alipohitimu miaka saba, baba alifariki na hakuna aliyejitolea kuwafariji kwa kupoteza baba .

Anachofahamu ni kuwa ghafla aligundua baba hayuko tena , aliachwa mikononi mwa bibi au nyanya.

Anasema binamu wake alimtishia kumuua ikiwa angetoboa siri iliyokuwa inaendelea mle nyumbani

Baada ya mazishi ya baba yake, baadhi ya ndugu za baba, mfano binamu wa baba na wajomba walianza kuishi kwao na kuendelea na masomo yao .

Celine anasema binamu huyo alikuwa na miaka kati ya 25-26 kitu kilichoanza kama tabia ya binamu wa baba kumtomasa kiliendelea kuwa kitendo cha kila siku cha unajisi na alimtishia kumuua ikiwa angetoboa siri iliyokuwa inaendelea mle nyumbani.

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Unywaji duni maziwa unaoelemewa na janga la wauzaji wanaochakachua



Mnywaji maziwa ya ng'ombe na lishe hiyo katika picha tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Ester Mgidula,** UDSM

UNYWAJI maziwa unasisitizwa na wataalamu wa afya, pia Shirika la Afya Duniani (WHO), kwamba walau kila mtu kunywa wastani wa lita 200 za maziwa kwa mwaka. Ni sawa na wastani wa glasi zisizoungua mbili kwa siku moja.

Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) inafafanua kwamba, kwa sasa nchi inazalisha zaidi ya lita bilioni 2.4 kila mwaka, huku wastani wa unywaji maziwa yenyewe kitaifa kwa mwaka ni lita 47, hali inayotafsriwa kuhatarisha afya ya umma.

Kunaweza kukawapo swali hata la mzaha uliobeba ukweli, kwamba unywaji unaendana na faida zipi? Wataalamu wa afya wana orodha yaa mlolongo wa kuwapo vitamini kama A, B, E na K, huku yakilainisha ngozi, kuimarisha meno na mifupa kutokana na uwepo wa madini ya 'calcium' na inaongeza nguvu za mwili, huku ikisaidia kupunguza uzito uliokithiri.

Kutokana na faida hizo, wanapendelea kutumia maziwa, ingawa kwa sasa ni faida iliyogeuka hasara, baadhi wanatumia maziwa yasiyofaa kiafya, huku baadhi ya wauzaji maziwa jijini Dar es Salaam wanaangukia taarifa zisizofurahisha kushuka soko.

> **Vilevile, kwenye maziwa ya mtindi kuna baadhi ya wauzaji ambao hutuuzia maziwa ya mtindi yaliyochanganywa na unga wa ngano...**



Inaelezwa, tabia ya wauzaji wengi kuchanganya maziwa na maji, tendo linaloangukia msamiati 'kuchakachua" huku kukiwapo wanaochanganya maziwa ya unga na ngano, kuongeza uzito baada ya kuchanganywa na maji.

Muuzaji mmowajapo wa eneo la Ubungo Mawasiliano, jijini Dar es Salaaam anayekataa kuandikwa jina, anakiri kuhusika na hujuma hizo akijitetea kwa ufafanuzi:

"Maziwa yana faida ndogo sana, hivyo bila kuzimua huwezi kupata faida uliyoitegemea. Kwa upande wangu, huwa nachanganya maziwa na maji, yaani kwenye kila lita moja ya maziwa ninaongeza maji kikombe kimoja ili nipate maziwa mengi mengi."

Anasema kwamba huwa anatumia lita tano nayompa faida ya Sh. 4500, kila glasi anauza kwa Sh. 1000 kulingana na ukubwa wa glasi hiyo, lakini anapochanganya, anapata faida zaidi inayosaidia ugumu wa maisha.

Katika ufafanuzi huo, mteja wake anayejitambulisha kwa jina Baraka Chande, mkazi wa Ubungo Kibo, ana maelezo yake:" Baadhi ya maziwa ukinywa huwa hayana ladha ya maziwa halisi, kutokana na kuwa yamechanganywa na maji kisha kuongezwa maziwa ya unga.

"Vilevile, kwenye maziwa ya mtindi kuna baadhi ya wauzaji ambao hutuuzia maziwa ya mtindi yaliyochanganywa na unga wa ngano na hii kwa wale wauzaji ambao wanapitisha barabarani."

**DAKTARI JE?**

Katika kupata ufafanuzi huo, mtaalamu wa afya Dk. Remijus Kibiki, anayejitambulisha mtumishi katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mkoani Kagera, anasema kuna athari inayopitia uchanganyaji maziwa na vitu vingine:

"Uchanganyaji wa maziwa kitaalam unaitwa 'adulteration.' Uchanganyaji huo hupunguza thamani ya maziwa kwa kuondoa virutubisho muhimu na athari yake kiafya inaitwa toxicological effects," anasema Daktari Kibiki.

Anafafanua kuwa maziwa ya unga yametengenezwa kwa malengo mahsusi, baadhi ni kwa ajili ya watoto na mengine watu wazima, hivyo uchanganganyaji wake unaweza kumletea madhara makubwa mtumiaji.

Daktari huyo anaendelea: "Maziwa mengine huwa yameharibika kutokana na kupitwa na wakati. Kwa hali ilivyo sasa, inaonyesha kuwa lengo la wafanyabiashara kuamua kuchakachua maziwa hayo, ili wapate faida kubwa, bila ya kujua kwamba wanaua soko la maziwa na wakati huohuo wanahatarisha afya za watumiaji."

"Nimeguswa sana na jambo hili, kwa sababu hivi sasa uuzaji wa maziwa umekuwa holela, kila mtu anauza bila ya kuzingatia ubora wa maziwa anayoyauza. Kwanini tupoteze afya zetu kwa mambo madogo kama haya?

"Kama hali hii itaendelea, tutauua kabisa soko letu la maziwa, Ifike wakati sasa tuelimike. Nchi yetu imeingia kwenye uchumi, hata uzalishaji wetu hauna budi. Tuachane na ujanja ujanja, ambao huwaondolea uaminifu hata kwa wale wauzaji wazuri wasiofanya."

Hivisasa, maziwa yanayoonekana kuaminika miongoni mwa jamii ni yanayosindikwa viwandani, ambayo kwa hali halisi ni ngumu kumudu gharama zake ndani ya uchumi wa mtu mmoja mmoja.

# MASAHIBU YA KUSHANGAZA

**INATOKA UK.11**

Anasema, hakujua wa kumgeukia, tabia yake ilibadilika mno na akawa msichana mtukutu na mwenye vituko . Hakuna mtu aliyeelewa, ni kwanini alikuwa na tabia za usumbufu.

Celine anasema alikuwa anaona aibu kumweleza mtu yeyote , hata bibi hakufahamu kuwa Celine alikuwa anapitia masaibu ya ubakaji kila siku.

Kitendo hicho kiliendelea tangu akiwa miaka minane hadi 14 hadi wakati binamu wake aliondoka kule nyumbani kwao na ilisalia kuwa siri

Kushika Mimba

Celine alipohitimu miaKa 15 alianza uhusiano wa kimapenzi na kijana mmoja . Mwanadada huyu anasema kuwa kwa mara ya kwanza alihisi kupendwa , mara tu alishika mimba na akajifungua mtoto wa kwanza akiwa na miaka 16.

Maisha yalibadilika mno , alitelekezwa na walezi wake , na akaanza maisha ya malezi ya mtoto . Uhusiano wake na yule baba ya mtoto uliharibika wakati huo .

Mtoto alipofikisha mwaka mmoja na miezi kadhaa Celine na yule mpenzi wake walirudia mapenzi tena na akiwa na miaka 17 alijipata ujauzito wa pili .

Kipindi hicho baba ya watoto wake wawili alifanikiwa kusafiri Marekani kwa ajira, lakini wakati huo alikuwa anatuma fedha za matumizi kwake Celine .

Baada ya miaka miwili baba ya watoto alirejea kutoka Marekani, waliamua kuanza maisha kama mke na mume , na hata Celine alishika mimba ya tatu , ila mambo yalikuwa tofauti . Mume wake alikuwa hajali , kwa mfano alikuwa na tabia ya kuwaleta wapenzi wengine ndani ya nyumba yao

Maisha ya kuwalea watoto wake hayakuwa rahisi na ndipo alihamia mtaani au kwenye nyumba ambazo hazina watu na, Februari alifunga ndoa na mume aliyekubali kuhudumia wanawe. **BBC**

AFYA

# Majaribio ya chanjo corona chuo kikuu Marekani yazua wasiwasi

**Na Nimi Mweta**



Mtaalamu wa Russia akiwajibika na kinga ya Covid 19. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

WASIWASI umetanda kiasi fulani katika anga za utafiti wa chanjo ya gonjwa la corona baada ya kulazimika kusimamisha majaribio hatua ya pili ya chanjo inayotayarishwa na kampuni ya AstraZeneca.

Inafanya kazi na wataalamu Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza na ni moja ya tafiti zilizokuwa zinaonyesha matumaini makubwa na sasa , hivyo hitilafu hiyo inaleta maswali lukuki.

Licha ya jitihada za kupata chanjo zinaendelea kwa kasi, ushawishi na matumaini sasa vinaanza kupungua, ukilinganisha na hali ilivyokuwa miezi kadhaa iliyopita.

Bado watafiti na wachunguzi wa habari walikuwa 'wanajitafuta' nini hasa labda kiliharibika katika utafiti wa Oxford na kampuni ya AstraZeneca. Kilichotangazwa mapema ni kuwa majaribio ya awali yameonyesha kuwa wanaopokea chanjo hiyo, au baadhi yao katika mazingira fulani ya viini au ngazi za ugonjwa kama upo - zinaleta hali hatarishi katika ngazi fulani.

Hapo ina maana kuwa usalama wa chanjo hiyo ndiyo umetiliwa shaka, licha ya kuwa uwezo wake wa kupambana na ugonjwa unapoingia mwilini, inawezekana hauko shakani na hawakukatishwa tamaa.

**MATUMAINI YALIKO**

Shirika la Utangazaji la Sky News nchini Uingereza, liliripoti kuwa maofisa wa juu katika utawala wa Rais Donald Trump nchini Marekani, bado wanaitumaini chanjo hiyo itakamilika na kuanza kutumika kwa wakati.

Ni moja ya maeneo ambayo Rais Trump, amekuwa akiwapa matumaini wananchi wa Marekani kuwa inawezekana kabisa kabla ya uchaguzi kufanyika Novemba 3 chanjo ikawa, tayari imeanza kutumika.

Dili za kutengeneza mamilioni ya vichupa vya chanjo tayari zilishafikiwa na nchi kadhaa duniani na mifuko ya kuchangia ununuzi kuanzishwa. Baadhi ya wataalamu kwa mfano katika mtandao wa ABC. Net, walisema majaribio ya chanjo kwa kawaida yanachukua hata miaka na huwa na vikwazo vingi kabla ya kukamilika.

Cha ziada walichosema ambacho chabashiriwa hakitasaidia kuleta au kuongeza matumaini kwa utawala wa Trump na kwingineko duniani, ni kwa wastani wa asilimia 90, majaribio ya chanjo huwa yanakwama hatimaye, na siyo tu kuwa na vikwazo katika kukamilika kitaaluma.

Kwa vile nchi zote kubwa kiuchumi ziko mbioni kutafuta chanjo, hajajulikana wa kufanikiwa uwezekano wa chanjo tarajiwa ya AstraZeneca kuwa na matatizo ya kina ulishaonekana wakati uliopita.

Mfano, gazeti la nchini India la Hindustan Times, lili andika habari kutoka nchini Ujerumani mwezi Julai, likisema kuwa chanjo tarajiwa ya AstraZeneca zilishindwa kuwaridhisha wataalamu huko. Ni kina cha cha maswali na majibu kuanza sasa.

> **Tumaini kimsingi, likawa limewekwa katika kupatikana kwa chanjo, ikiwezekana kabla ya uchaguzi, lakini haikuwa inatazamiwa kuwa ingekuwa mapema mwezi Septemba.**

Waliofuatilia suala hilo zaidi walishangaa kuona kuwa hata mwezi Mei, miezi miwili kabla ya taarifa hiyo kutoka Ujerumani, tayari maswali ya uhakika wa kupata chanjo kwa jitihada za AstraZeneca yalikuwa yameanza kutanda.

Wapo nchini Uingereza wanaohofia kuwa mikataba ya kibiashara ya kupatikana kwa chanjo hiyo ambayo ilishaanza na nchi kubwa kadhaa duniani, wakiikimbilia chanjo hiyo tarajiwa. Maoni yao ni utafiti ulitakiwa kuendelee na si kuwahi majaribio.

**KUTOKA RUSSIA**

Hakuna uhakika kama chanjo tarajiwa ya Russia, ilipata baraka za serikali ya nchi hiyo kuanza kutumika imepita ngazi zote au kufanyiwa majaribio ya kina nchi za Magharibi hadi sasa.

Kimsingi, bado usahihi wake kwa maana ya ustadi wake kitaaluma haujahojiwa kwa nguvu. Baada ya serikali ya Russia kutoa idhini kuwa ianze kutumika hasa katika jeshi la nchi hiyo, kabla ya kuenezwa kwa raia na kuanza kuuzwa nje.

Mapitio ya awali yaliyochapishwa katika jarida moja la kitaaluma yaliashiria kuikubalii chanjo hiyo kwa wakati huu. Ina maana hakuna tatizo lolote lililogunduliwa hadi ianze kutumika rasmi Russia.

Kwa utawala wa Rais Trump, hizo zitakuwa habari mbaya tatu katika jitihada zake za kupata kinga au chanjo ya corona kwa haraka iwezekanavyo.

Hatua ya kwanza, ni kuipigia debe dawa iliyotangazwa rasmi mwezi Juni kuwa haina nguvu ya kutibu wagonjwa wa corona.




Dawa ya kinga dhidi ya maradhi ya Covid 19, iliyofanyiwa majaribio katika Chuo Kikuu, nchini Uingereza.

Wiki chache zilizopita Rais Trump alikuwa anapigia debe waliowahi kuugua na kupona corona wajitokeze kutoa damu, ili itumike kusaidia wale ambao wamepatwa ugonjwa huo kujenga kinga na kupona.

Hiyo nayo muda si mrefu 'ikapigwa chini' kuwa kinga ya mtu mmoja haimsaidii mwingine haraka.

Tumaini kimsingi, likawa limewekwa katika kupatikana kwa chanjo, ikiwezekana kabla ya uchaguzi, lakini haikuwa inatazamiwa kuwa ingekuwa mapema mwezi Septemba.

Hiyo ina maana kuwa kwa hali yoyote ile, chanjo ya AstraZeneca ilikuwa haijawa tayari kwa majaribio ya kina, na hivyo tatizo liloonekana ni la kawaida kwa dawa ambayo bado haijakamilika. Lakini, ilivyotangazwa ilikuwa tofauti, kama vile kuna kitu kilichoharibika, ambacho kimsingi katika utafiti wa chanjo hiyo.

Katika mazingira yaliyopo hivi sasa, ni rahisi Russia bado ndiyo inachanja mbuga na chanjo ambayo imefanyiwa majaribio ikawaridhisha wataalamu nchini humo na wakaithibitishia serikali kuhusu ubora wake.

Hadi sasa halijakanushwa na watafiti au wachunguzi wa habari wa nchi nyingine na hasa za Magharibi, hali inayoonyesha chanjo hiyo ya Russia inaweza kupata soko kubwa tena haraka kwani katika nchi za Magharibi, ni utafiti wa AstraZeneca, uliokuwa unawekewa matumaini zaidi.

Hata hivyo, China ilikuwa imeanza majaribio ya chanjo ya Sinovac nchini Indonesia wiki ya pili ya Agosti, lakini ilikuwa katika mazingira kama ya AstraZeneca, kuwa bado iko katika hali ya 'kupikwa' na haijaonyesha ukamilifu wa 'Sputnik V' ya Russia.

MAZINGIRA

# Nishati mbadala na madini adimu, dhidi ya uharibifu mpya mazingira



Ukanda wa machimbo ya bati, nchini Chile.

**Na Nimi Mweta**

WAKATI dunia imeshaamini kuwa dawa ya kuondoa uchafuzi wa mazingira, ni kuacha kutumia makaa ya mawe na mafuta mazito, petroli, dizeli na badala yake kuhamia nishati mbadala wataalamu lukuki wamekuwa wakifundishwa kuwa ni endelevu, ushawishi huo sasa unaanza kufifia.


Chanzo cha kupauka kwa dhana hiyo ni vifaa vinavyohitajiwa hasa kwa ajili ya kutengeneza 'pangaboi' za nishati upepo na vifaa vya umeme jua, kama ilivyo matumizi mengine ya vifaa vya kielektroniki, kuwa vifaa vinategemea aina kadhaa za madini adimu. Upatikanaji wake una madhara balaa.

Imepita miaka kadhaa, wataalamu wa mwelekeo tofauti wamekuwa wakiibua maswali kuhusu uendelevu wa nishati mbadala, baada ya madhara kuanza kutajwa katika maeneo yanayopatikana madini ya kutengeneza vifaa hivyo.

Hivi karibuni, televisheni moja ya kimataifa ilitoa makala ya utafiti kuhusu uchimbaji bati na madini adimu yanayofanana na hayo nchini China, na ile ya shaba nchini Chile, ikionaisha na uharibifu 'wa kutisha' wa mazingira unaoonekana katika nchi hizo, huku mamlaka nyinginezo za usimamizi mazingira zinakiri hayo.

Zipo taasisi kadhaa zenye uhusiano na mazingira, zilizoanza kuchipua katika nchi za Magharibi kusambaza na kutafiti zaidi hoja dhidi ya kile kinachoitwa nishati mbadala.

Mtazanmo ulioko ni kwamba, matazamio ya dunia ni kujikomboa na mafuta kutokana na uzalishaji hewa aona ya 'carbon dioxide' au ukaa, utatuzi wa suala zima la mazingira na bomu la kutegwa.



Sehemu ya machimbo ya bati nchini China. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Sera za kiharakati za nishati mbadala zimeharibu usimamizi na tija katika utengenezaji na usambazaji wa umeme jimboni humo.**

Kwa kuhamia nishati mbadala, dunia sasa inaingia katika utegemezi mpya wa vyuma adimu ambavyo upatikanaji wake kwa viwango vya kutosha na hasa kwa bei inayofaa ni mkasa kimazingira. Inaacha maswali ya ujio wa 'dunia ya kijani.'

Tatizo la nishati endelevu katika utafiti huo ni jinsi takriban kila kinachohitajiwa katika nishati za upepo, umeme wa jua na zile za mimea (baioanuwai) siyo 'nishati safi' au ya 'kijani' hata kidogo.

### CHILE & CHINA

Makala ya televisheni moja, ilionyesha maeneo makubwa ya jangwa ambako uchimbaji wa bati na shaba unaotumia maji mengi ya kawaida umeharibu kabisa vyanzo vya maji sehemu kubwa tu za China na Chile. Katika eneo la 'jangwa la shaba' huko Chile, walisema haijanyesha mvua kwa miaka 500 sasa.

Ina maana, mtu akiangalia kwa karibu, ni rahisi zaidi kwa dunia kutafuta njia za kukabiliana na athari za matumizi ya makaa ya mawe na mafuta ya kuchimbwa, kuliko kutegemea upatikanaji kwa wingi vyuma adimu.

Pia, umeme wa nishati mbadala unaonekana kukosa tija ya kutosha kubadili nafasi ya mafuta na nyuklia, kwa sababu unahitaji vifaa vingi kwa uzalishaji mdogo wa umeme, pale inapolinganishwa na umeme wa maji au mafuta.

### UMEME MBADALA

Umeme mbadala umetumika katika maeneo kadhaa yenye uhitaji wa umeme kwa kiasi tu yaliyoko mbali na njia za umeme wa kawaida, wa mafuta au maji.

Kwanza, vifaa vya kutafutia madini ya vyuma adimu ambavyo vinatumika kusuka 'jenereta' za umeme mbadala, hasa mashine za uchimbaji wa madini hayo na usafirishaji wake kimsingi vinategemea matumizi ya mafuta ya kawaida na mafuta mazito.

Ina maana hapatakuwa na afueni ya wazi au haraka, kwani matumizi ya mafuta yanayozalisha gesi chafu yatabadilika kiasi kidogo, lakini hayakwepeki katika kazi kuu za kuzalisha nishati au utafutaji madini. \

Kinachoongezeka ni hitaji kubwa la madini adimu kama chuma na bati, ambayo yanaharibu mazingira kuliko mafuta.

Kikundi kimojawapo cha watafitii nchini Marekani, kinafafanua kwamba, betri moja ya gari la kawaida linalotumia umeme badala ya petrol au dizeli ina uzito wa karibu nusu tani.

Hivyo, ili kutengeneza betri hiyo, kunabidi kuchimbwa na malighafi ardhini yenye uzito mara 500 ya hiyo betri, 'kutoka popote pale katika sayari ya dunia.'

Pia, kuna sura ya pili ya ntazamo kwamba uchimbaji wa madini hayo, ikiwemo afya za wafanyakazi katika mazingira ambayo kuchimba unalenga kuuza madini hayo kwa bei ya chini kabisa, kwa mfano inavyofanya China kutawala soko, ni jambo ambalo mikutano ya mazingira haina habari.

Kinachoonekana ni kikwazo kikubwa zaidi cha nishati mbadala na hasa kwa kutengenezwa vitu 'vinavyong'ara' ni wingi wake na uunganishaji kila mahali, kwa mfano gari la umeme kuhitaji nyaya za umeme njia yote inayopitia, si sawa na kujaza mafuta mara moja.

Maoni mengine ni namna vyuma vya kawaida vya magari vinayeyushwa na kutumika kutengeneza vifaa vya chuma au magari mengine, ikiwa si rahisi kukomboa na kuanza kutumia tena vingi ua kitaalamu 'recycling'kati ya malighafi au vifaa vya kielektroniki.

### DARASA LA MAREKANI

Mojawapo ya maeneo ya umeme mbadala yaliyofanyiwa utafiti hivi karibuni nchini Marekani, ni katika jimbo la California, ambako wataalamu wanasema jitihada za kutengeneza umeme mbadala kwa wingi zinakaribia kufilisi kampuni kubwa ya umeme eneo hilo.

Ni jimbo ambalo kwa miaka mingi linaongozwa na magavana kutoka chama cha Democratic wapinzani wa chama tawala.

Wanasema sera za kiharakati za nishati mbadala zimeharibu usimamizi na tija katika utengenezaji na usambazaji wa umeme jimboni humo.

Utafiti huo ni kwa jimbo linalopata malighafi hizo kutoka kwa baadhi ya nchi, ambazo hata sauti zake kuhusu uharibifu wa mazingira hazifiki mbali, labda kwa kusaidiwa na wanahabari.



# Maliasili kuandaa maadhimisho miaka 100 ya Nyerere

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeanza kuandaa maadhimisho ya miaka 100 tangu kuzaliwa kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kwa kukusanya kumbukumbu zake ili kuwa vivutio vya kitalii.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aloyce Nzuki, alisema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa kupokea taarifa kutoka wizara na idara mbalimbali.

Alisema wizara imeandaa kamati maalum kutoka sekta na wizara mbalimbali ili kuainisha, kujadiliana na kupendekeza maeneo hayo kupanua wigo wa utalii nchini.

Alisema wizara hiyo imeanza mikakati upya ya kumuenzi Mwalimu Nyerere ili kuongeza baadhi ya kumbukumbu ambazo hazikuwapo kwenye vivutio vya utalii. Alitaja baadhi ya mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuziweka hotuba zake alizowahi kutoa maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi zitawekwa kwenye mfumo wa kidijitali ili kutumika kujifunza.

"Baadhi ya maeneo mengine yanayotakiwa kuingia kwenye kumbukumbu za utalii ni nyumba alizowahi kuishi maeneo tofauti nchini na shule alizowahi kusoma na kufundisha," alisema.

Alisema lengo la kuingiza kwenye vivutio vya utalii vya taifa na kuwavutia watalii wanaotembelea nchini kuangalia kazi zilizofanywa na viongozi maarufu.

Kadhalika, alisema kamati hiyo maalum itakuwa na jukumu la kuandaa maadhimisho ya miaka 100 ambayo yanatarajiwa kufanyika mwaka 2022.

"Baba wa Taifa alizaliwa mwaka 1922 hivyo kufikia mwaka huo 2022 atatimia karne moja yenye miaka 100 tangu kuzaliwa kwake," alisema.

Naye mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Madaraka Nyerere, aliishukuru serikali kwa kuanzisha mikakati hiyo ya kuweka kumbukumbu za Mwalimu Nyerere kwenye vivutio vya utalii pamoja na kushirikisha familia yake. Madaraka alisema maadhimisho hayo yalikuwapo, lakini sasa serikali imeona iyaboreshe na kuyaongezea baadhi ya vitu ambavyo havikuwekwa kwenye kumbukumbu.

Aliahidi kwa niaba ya familia yao kutoa ushirikiano na baadhi ya vitu ambavyo serikali itaona vizuri kuvichukua na kuviweka sehemu nyingine kwa ajili ya kuwa vivutio vya utalii.

Kwa upande wake, mwenyekiti wa kamati hiyo, Imani Kajula, alisema maadhimisho hayo yanalenga kumuenzi Mwalimu kutokana na kazi alizowahi kuzifanya katika uhai wake.

Alitaja lengo lingine kuwa ni kujenga misingi endelevu ya maadhimisho hayo kuendelea kusherehekewa kwa miaka mingi ijayo.

Pia, alisema kuwa maadhimisho hayo yanalenga kuipa umuhimu siku hiyo kutokana na kazi alizowahi kuzifanya ndani na nje ya nchi na alipigania na kuyasaidia baadhi ya mataifa kupata uhuru wao.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Joseph Sokoine (kushoto), akijadiliana jambo na Madaraka Nyerere, wakati wa kikao cha kamati iliyoundwa na Waziri wa Maliasili na Utalii kuandaa mkakati wa kuenzi kazi alizowahi kufanya Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere, ili ziingie kwenye vivutio vya utalii na kuandaa maadhimisho ya miaka 100 tangu kuzaliwa kwake, jijini Dodoma jana.
**PICHA: IBRAHIM JOSEH**

# NARCO yatumia mil. 300/- kuboresha mipaka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI ya Ranchi za Taifa (NARCO), imetumia zaidi ya Sh. milioni 350, kuboresha na kutengeneza mipaka mbalimbali ili kuepusha migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkurugenzi wa NARCO, Masele Mipawa, alisema mipaka hiyo imewekwa kwenye mikoa mbalimbali nchini na lengo ni kutaka wafugaji na wakulima wote wawe na maeneo ya kufanyia shughuli zao.

Alisema baadhi ya maeneo yaliyowekewa mipaka ni Misenyi, Ruvu, Uvinza, Taasisi za Jeshi la kujenga Taifa, Kiwanda cha sukari Kagera pamoja na maeneo mengine. "Sasa hivi hakuna tena migogoro inayosikika kila mmoja ana eneo la kuendeshea shughuli zake," alisema Masele.

Pia, alisema bado wanaendelea kutengeneza mipaka katika maeneo mbalimbali bila kuidhulumu jamii wala NARCO.

Hata hivyo, alisema wametenga hekta 22,200 kwa ajili ya vijiji na hatua hiyo imejenga urafiki baina ya NARCO na raia wanaoishi katika maeneo hayo. "Tumetenga maeneo kwa ajili ya vijiji lengo ni kuondoa kelele za kila siku ambazo watu hupigana kwa ajili ya ardhi, ardhi ni ya kila mmoja tunagawa kwa mipaka na kila mmoja anajua wapi anatakiwa akae kwa ajili ya kuendesha kazi zake," alisema.

Masele, alisema hivi sasa NARCO wanaona faida ya kutengeneza mipaka na hakuna migogoro wala watu kukatwa mapanga.

Vile vile, alisema utengenezaji mipaka utaendelea katika maeneo yote ambayo inastahili kuwapo ili kuwaweka wananchi sawa. Akizungumzia ubora wa vifaa, alisema hivi sasa wanavitendea kazi bora ambavyo wanavitumia kuhakikisha NARCO inakuwa bora. "Kila kitu NARCO kimeboreshwa, miundombinu, vitendea kazi kwa hiyo tumefanya mageuzi ya kutosha," alisema Masele.

Alisema, bidhaa zinazozalishwa na NARCO zina ubora na nzuri kwa matumizi ya binadamu.

Aliwataka wananchi kutosita kushirikiana na NARCO katika kuhakikisha wanajenga uhusiano.

# Chama cha Biblia chawajengea uwezo wananchi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Biblia cha Tanzania, kimewajengea uwezo wa kusoma na kuandika wananchi 248, ili kutambua fursa mbalimbali za kiuchumi.

Wananchi hao ni wa vijiji 13 vya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro na mpango huo uliandaliwa na chama hicho kwa kushirikiana na Chama cha Biblia cha Finland.

Mratibu wa programu hiyo kutoka chama hicho, Frank Makala, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa mpango huo na kuwapatia wahitimu vyeti vya elimu ya watu wazima.

Alitaja vijiji ambavyo vilivyonufaika na mradi huo wa kusoma na kuandika ni Nguyami, Berege, Chakwale, Ibindo, Mwandi, Mambiya, Mbili, Dumbaalume, Maguha, Magela, Kiegela na Mabula.

Alisema mradi huo ulilenga kuwafundisha kusoma na kuandika wananchi hao kuanzia wenye umri wa miaka 14 na kuendelea.

Alisema programu hiyo ni mwendelezo wa awamu ya kwanza iliyoanza mwaka 2017 yenye watu 120 walijiandikisha huku 97 ndio walihitimu kwa kufundishwa kwa lugha ya Chikagulu na kufanikiwa kuandika kwa Kiswahili.

"Chama cha Biblia cha Tanzania tunaishukuru serikali kutokana na programu hii, kwa kuwa imeanza kuwatambua na kuwaingiza kwenye mfumo wa MEMKWA katika shule za msingi kama ilivyoelekeza Wizara ya Elimu kwa ajili ya kujifunza zaidi," alisema.

"Sisi hapa Chama cha Biblia cha Tanzania kwa pamoja na Chama cha Biblia Finland tunawafundisha kusoma na kuandika tu ila huko watajifunza zaidi masomo mengine kama vile Hesabu, Sayansi, Jiografia na Historia."

Kwa upande wake, Canon Elias Chamwenya, ambaye alimwakilisha Askofu Godfrey Sehaba wa Dayosisi ya Morogoro, Kanisa la Anglikana kwenye mahafali hayo, aliwataka wahitimu kutumia maarifa hayo kwa kujiendeleza kiuchumi na kushiriki katika uchumi wa taifa.

Naye Meneja wa Miradi na Utunishaji mfuko wa Chama cha Biblia cha Tanzania, Samweli Mshana, ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Chama hicho, Alfred Kimonge, alisema lengo la chama hicho ni kutafsiri lugha za asili, kukuza na kutunza pamoja na kusaidia jamii husika kujua kusoma na kuelewa neno la Mungu.

Mmoja wa wahitimu, Raheli John, alisema mradi huo umewasaidia kujua kusoma na kuandika tofauti na awali walikuwa wakilazimika kuomba msaada wa kusomewa na kuandikiwa.



# Wakulima pareto watoa ya moyoni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa pareto katika Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwapatia elimu itakayowasaidia kuzalisha mazao yenye sumu nyingi na inayohitajika kwenye soko.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema mara nyingi wanunuzi wa zao hilo wamekuwa wakichukua mazao yao na kwenda kupima kiwango cha sumu kwenye maabara ambazo hawana uwakilishi wowote na malipo wanayoletewa huwa ni kidogo kwa kisingizio kuwa kiwango cha sumu kiko chini.

Mmoja wa wakulima wa Kata ya Simambwe, Yusuph Butusyo, alisema hawajawahi kupewa elimu na juu ya njia bora za uzalishaji wa zao hilo ambazo zitawawezesha kuzalisha mazao yenye sumu nyingi kuliko wanayozalisha kwa sasa.

Alisema mara nyingi huwa wanapata elimu kutoka kwa wanunuzi na kwamba wakati mwingine huwa wanashindwa kuiamini elimu wanayopewa kwa sababu wanunuzi hao huwa wanawapunja kwenye malipo kwa kisingizio cha sumu.

"Tunaomba serikali itusaidie wataalamu wa kutupa elimu ya uzalishaji bora wa pareto, kwa sasa tunatumia uzoefu tu na pengine tungepata wataalamu tungefaidika zaidi na zao hili kiuchumi," alisema Shila.

Alisema mnunuzi mkuu wa pareto katika wilaya hiyo huwa anakwenda nazo Mufindi mkoani Iringa ambako ndiko kwenye maabara ya kupimia kiwango cha sumu.

Naye Sophia Mwazembe, alisema bei wanayouzia zao hilo kwa sasa ni ndogo ikilinganishwa na gharama wanazotumia kwenye uzalishaji hali ambayo inawafanya baadhi kuanza kukata tamaa ya kuendelea kuzalisha.

Alisema kwa sasa wanauza zao hilo kwa Sh. 2,400 kwa kilo tofauti na maeneo mengine yanayozalisha zao hilo duniani ikiwamo nchi jirani ya Kenya ambayo alidai bei huwa inafika mpaka Sh. 5,000.

"Kuna baadhi ya wenzetu wameng'oa miche ya pareto kwenye mashamba yao na wameanza kupanda miti na wengine wanaamua kulima mazao ya chakula kama mahindi na maharage," alisema Mwazembe.

Alisema kuna kipindi waliaminishwa na viongozi wa kisiasa kuwa kiwanda cha kuchakata zao hilo katika ukanda huo, lakini mpaka sasa dalili hazionekani hali ambayo inawafanya waendelee kutegemea mnunuzi mmoja.

# Mgombea ubunge ajitwisha mgogoro wananchi, TANAPA

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Liberatus Mwang'ombe, amewakumbusha wananchi kumchagua kiongozi ambaye atakubali kubeba na kutatua vikwazo vinavyowakabili ikiwamo mgogoro wa muda mrefu baina ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na baadhi ya vijiji.

Mwang'ombe alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa kampeni katika Kata ya Ubaruku, huku akisema wananchi wanapaswa kuwa watulivu katika kuchagua viongozi ambao watakubali kubeba jukumu hilo.

Alisema moja ya masuala atakayoyafanya iwapo atachaguliwa ni pamoja na kushughulikia suala hilo kwa kuwa atakuwa sehemu ya watunga na wapitisha sheria bungeni.

Pia alisema suala lingine la kipaumbele ni kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo na ufugaji ili kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

"Kiu yangu ni kuona wana Mbarali wanaishi kwa uhuru. Nitahakikisha nashughulikia masuala yote yahusuyo migogoro ya ardhi baina ya hifahi na vijiji, mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali na wakulima," alisema Mwang'ombe.

Aliongeza kuwa endapo atapata ridhaa ya kuwaongoza Wanambarali atahakikisha huduma za mama na mtoto zinatolewa bure kwenye vituo vyote vya kutopewa huduma, sambamba na uboreshaji wa mfumo katika utoaji mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Alisema Ilani ya CHADEMA inavyoelekeza kuhusu utoaji wa huduma za afya kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ataitekeleza kwa vitendo sambamba na kuhamasisha ujenzi wa hosteli kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike kusoma kwa utulivu na kutimiza ndoto zao.

Sambamba na hilo, aliahidi kuyasaidia makundi maalum mikopo yenye masharti nafuu na mazingira bora ya upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

Hivi karibuni mgombea urais kwa tiketi ya chama hicho, Tundu Lisu, akiwa mkoani Mbeya, aliwaahidi wananchi kuwa endapo atapata ridhaa ya kuwaongoza Watanzania, atahakikisha anaboresha uchumi pamoja na huduma za afya.



Mtafiti wa mboga na matunda kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Uyole, Daudi Mbongo (kushoto), akitoa maelekezo kuhusu namna ya kuotesha mbegu za parachichi kwa mkulima, Ali Mohamed katika Mtaa wa Mahenge mkoani Ruvuma, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wazee waomba kasi upatikanaji dawa

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAZEE wa Kata ya Rujewa wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuongeza kasi ya upatikanaji wa dawa kwenye dirisha la wazee.

Kwa kufanya hivyo, kutawafanya kuwa na uhakika wa kupata matibabu kuliko ilivyo sasa kwa kuwa baadhi ya dawa hazipatikani.

Katibu wa Wazee Rujewa, Christina Mwalyaje, aliyabainisha hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wazee ambayo yalifanyika kiwilaya katika Kata ya Rujewa.

Alisema wanapofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, wahudumu hudai dawa zimekwisha hivyo wakanunue kwenye maduka ilhali baadhi yao hawana uwezo wa kumudu gharama za kununua.

Kutokana na tatizo hilo kwenye vituo, alisema wanaiomba ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, kumteua mtu maalum ambaye atashughulikia suala hilo ili kuwasaidia kupata matibabu ya uhakika.

Sambamba na hilo, alisema pia mtu atakayeshughulikia suala la wazee kupata dawa zinazohitajika, ahakikishe anaweka utaratibu wa kupunguza foleni na milolongo mingine ili watibiwe haraka.

Alieleza moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo wazee ni pamoja na baadhi ya wagonjwa wengine kutumia dirisha hilo kupata matibabu.

"Naamini suala la upatikanaji wa dawa likishughulikiwa kwa ufanisi, wakaweka utaratibu wa utoaji huduma hakika afya zetu sisi wazee zitaimarika. Jambo la msingi ni kuwaomba watendaji wanaotoa huduma za afya kutomwangusha Rais wetu kwa sababu amewekeza fedha nyingi sana kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee," alisema Mwalyaje.

Akizungumzia suala la uwakilishi wa wazee kwenye vikao vya uamuzi, alisema wanaomba wazee washirikishwe kwenye vikao mbalimbali.

Mmoja wa wazee katika maadhimisho hayo, Juma Michael, alisema kundi hilo linapaswa kuangaliwa kwa jicho la kipekee kwa sababu wana mchango mkubwa katika kuliletea taifa maendeleo.

Alisema miongoni mwa masuala yanayotakiwa kuboreshwa ni uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya na maji kwa sababu ni maeneo yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja.

Aidha, aliishauri serikali kuwa Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 itungiwe sheria ili wazee watunzwe kama sera ilivyoandikwa pamoja na kupatiwa mikopo nafuu, ili kujikwamua na kuishi maisha yenye ustawi.






Mgombea wa urais kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akihutubia wananchi wa majimbo ya Kiwani na Chambani katika mkutano wa kampeni kwenye viwanja vya Mauwani Kiwani Mkoa wa Kusini Pemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi aahidi viwanda kuongeza thamani karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema akichaguliwa kuwa rais anakusudia kuweka miundombinu bora ikiwamo kujenga viwanda vitakavyoongeza thamani ya zao la karafuu na wakulima kupata kipato zaidi.

Dk. Mwinyi alisema hayo wakati akizungumza na wakulima wa karafuu wa mikoa miwili ya Pemba na kwamba anakusudia kumaliza malalamiko ya wakulima wa zao hilo kuhusu kasoro za vipimo wakati wanapouza.

Alisema anataka kuona wakulima wanazalisha karafuu na kufikisha tani 10,000 kutoka tani 8,277 huku wakifaidika na ongezeko la thamani ya zao hilo kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali.

"Najua uzalishaji wa karafuu umekuwa ukiongezeka hatua kwa hatua...kwa mfano katika mwaka 2015 mliweza kuzalisha tani 3,321 na katika mwaka 2018 mlizalisha tani 8,277, lakini nikiingia madarakani nataka mfikie kiwango cha uzalishaji tani 10,000," alisema.

Akitoa habari njema kwa wakulima wa karafuu katika kisiwa cha Pemba alisema anakusudia kutoa mikopo nafuu kwa wakulima pamoja na pembejeo, ili kuyafikia malengo hayo na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Alisema sio sahihi kwa mkulima wa karafuu au mazao ya viungo anapotaka mkopo kupewa masharti ya kupeleka waraka wa nyumba kama ithibati ya kupata mkopo. "Nikichaguliwa kuwa rais nitazungumza na taasisi za fedha zikiwamo benki kuona wanatoa mikopo nafuu kwa wakulima wa karafuu na mazao ya viungo na wakati mwingine serikali iwe ndiyo dhamana ya mikopo hiyo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya wakulima wa karafuu, Pemba Sharif Maalim, alisema bado wakulima wana manung'uniko ya kupunjwa kwa vipimo wakati wanapouza karafuu zao katika vituo vya Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC).

Alisema kwa upande wa mikopo inayotolewa ZSTC imekuwa na urasimu mkubwa.

"Tunakuomba ukifanikiwa kuingia madarakani na kuwa rais wa Zanzibar tunataka ulifanyie kazi tatizo la wakulima kupunjwa karafuu katika suala la vipimo... hatujaridhika na vipimo," alisema.

## Maalim Seif kuunda Jeshi la Polisi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema endapo wananchi watampatia ridhaa ya kumuweka madarakani ataunda Jeshi la Polisi la Zanzibar.

Maalim Seif aliyaeleza hayo huko Mkoa wa Kusini Pemba katika Jimbo la Kiwani katika mwendelezo wa kampeni zake za urais.

Alisema wakati huu wa vuguvugu la siasa imekuwa kawaida viongozi wao kukamata, lakini wakifika kituoni huhojiwa na askari kutoka Tanzania Bara na kudai hilo litafika mwisho maana akiingia Ikulu ataunda jeshi lake la polisi.

Alisema Zanzibar kukosa Jeshi la Polisi, kunasababisha vijana wengi kukosa ajira kwa sababu wanaonekana wapinzani.

"Nitaanzisha jeshi letu wenyewe hapa na Zanzibar itakuwa na mamlaka kamili ya kutenda tunalolitaka," alisema Maalim Seif.

Maalim Seif alisema kwa upande wa Muungano baada ya kuchaguliwa kuwa rais atazungumza na Rais wa Jamhuri kukubaliana upya kuhusu mambo ya Muungano.

Alisema hivi sasa wananchi wa Zanzibar wanaonekana kama raia, kutokana na nchi yao kukosa utambulisho wa dunia.

"Hawa washajiona hawana kura tena katika Visiwa vya Zanzibar lililobakia ni kutisha wafanyakazi na wazee," alisema.

Pia atahakikisha ameirudisha Benki Kuu ya Zanzibar ili waweze kudhibiti fedha zao.

Hata hivyo, alisema kuwa katika serikali yake wazee watalipwa zaidi ya laki moja kwa mwezi ili na wao watumie maendeleo vizuri ya nchi yao.

# Mgombea urais AFP asisitiza kulinda amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha AFP-Wakulima, Said Soud, amewataka wananchi wa kisiwa cha Pemba wasikubali kudanganywa na kuvunja amani ya nchi ambayo ndiyo maisha ya wananchi katika kupata maendeleo.

Soud alisema hayo wakati akizindua mkutano wa kampeni huko Wawi, Pemba na kwamba wapo viongozi wameanza kuwashawishi wananchi kuingia katika vurugu za kisiasa kwa kuona wameanza kupoteza mwelekeo wa kisiasa.

Alisema wananchi wa kisiwa cha Pemba wanazifahamu athari za uvunjifu wa amani na katika mwaka 2000 vurugu za kisiasa ziliibuka na kusababisha watu kadhaa kupoteza maisha na wengine kuvikimbia visiwa hivyo na kuishi Mombasa Kenya. "Wananchi wa kisiwa cha Pemba msikubali kutumiwa kisiasa kwa kuhatarisha amani na utulivu...thamani ya nchi ni amani kwa ajili ya kuleta maendeleo," alisema.

Alisema akichaguliwa kuwa rais anakusudia kulifufua upya eneo la ukanda wa uchumi wa maeneo huru ya uchumi Micheweni, ili kujenga viwanda vingi vikiwamo vya kusindika samaki.

Alisema hadi sasa kisiwa cha Pemba licha ya kuzungukwa na bahari sehemu zote, lakini hakuna kiwanda cha kusindika samaki ambacho kitawawezesha wavuvi kuongeza uzalishaji.

"Nikichaguliwa kuwa rais nataka kujenga viwanda vingi vya kusindika samaki ambavyo vitawawezesha wavuvi kuongeza uzalishaji wa samaki," alisema. Kwa upande wao wagombea wa nafasi ya ubunge na uwakilishi Jimbo la Wawi, wameomba wananchi wawachague ili wapate nafasi ya kutatua changamoto zinazowakabili ikiwamo huduma za maji.

"Nawaomba wapigakura wa Jimbo la Wawi nichagueni ili nizipatie ufumbuzi changamoto zinazowakabili ikiwamo tatizo la majisafi na salama," alisema Sahaibu Hassan, mgombea wa nafasi ya uwakilishi.

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**BEACH PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 0.91 Acres (3682.64 Square Meters)
LOCATION: - PLOT NO 40, KUNDUCHI BEACH, NEXT TO SILVER SANDS,DARESALAAM CITY
DESCRIPTION: - DIRECT ACCESS TO THE BEACH.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

## VIWANJA/MASHAMBA

**Eneo linapangishwa/kuuzwa**
Eneo linapangishwa/ kuuzwa ukubwa wa mita mraba (sqm) 3,130, Tabata Liwiti, Dar es Salaam. Liko katika barabara kuu na inafaaa kwa ajili ya kujenga kituo cha mafuta, super market nk. Wasiliana kwa simu: 0715624747/0767235965.

## VIWANJA/MASHAMBA

**PRIME PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 14.87 HECTARE (36.74 ACRE)
LOCATION: - BAGAMOYO DISTRICT, BLOCK C SANZALE, LOCATED ON MAIN ROAD, 5 MIN FROM BAGAMOYO TOWN,3 KM AWAY FROM ROUND ABOUT
DESCRIPTION: - THE PLOT IS FURTHER DIVIDED IN 5 DIFFERENT TITLES.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



115924102

**EDWIN THIMOTH NDUNGURU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.143/53** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NJOMBE SEKONDARI mwaka 1984. Cheti cha Chuo cha Reli Tabora kilichotolewa mwaka 1988. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/356569/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115923302

**Mohamed U. Ashiru** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato sita chenye index namba **S0445-0649** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari Mwembetogwa. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DSM/PHQ/RB/698720/2020**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki wa Kampuni ya **VK Green Architects Ltd** yenye usajili wa **Brela no. 87055 wa 9/11/2011** inapenda kuutangazia umma kuwa kampuni yao imekuwa ikijiendesha kwa hasara na inafungwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni Brela. Mikataba yote inayoendelea ya kampuni hii itamaliziwa na Arch. Dr. Victoria Marwa Heilman kwa jina la biashara Alama Architecture yenye usajiri namba **475436** wa **21-07-2020.**

115923402

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 66 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU SAID JUMA ASSAD**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**KHALID JUMA ASSAD & OTHERS**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24 Mwezi wa Octoba, 2020.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 21 Mwezi wa Septemba, 2020.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI

115924302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**

**Mahakama ya Mwanzo ARUSHA –MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**

**MADAI NAMBARI 204/2020**

**Mdai JOSEPH BLASS MASSAWE**

**Mdaiwa FRANCIS ALFEI KIKA**

**Kwa FRANCIS ALFEI KIKA WA SINONI-ARUSHA.**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yako kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

**FIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADA YA TSHS 10,000,000/= BILA KUKOSA.**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya 6/10/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hili, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21/09/2020
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

21/9/2020

115924202

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**Samwel Yohana Machiya** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 231 BXM** aina ya **PIAGGIO.**
Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.
Taarifa ya Polisi: **KAH/TR/RB/332/2020.**

115923902

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA MTAA WA SARUJI TANGA, KATA YA MAWENI. IKO KWENYE KIWANJA **NO. 267 KITALU "A"** MAWENI **HATI MILIKI NO. 470522,** KINA UKUBWA WA **4320 SQM,** UMBALI WA KIASI CHA MITA 300 TOKA BARABARA KUU TANGA-KOROGWE-MOSHI, TANGA-DAR, KILOMETA 10 KUTOKA KATIKATI YA JIJI.

***MIUNDOMBINU YA MAJI NA UMEME YA UHAKIKA IPO.* NI ENEO ZURI LA UWEKEZAJI, KWA KUJENGA APPARTMENTS, UFUGAJI SAMAKI, NYUKI, KUKU N.K NA MAKAZI PIA.**

***HAKUNA DALALI;***

**TUPIGIE KWA IMANI NA MATUMAINI NAMBA 0713-330132, 0787-007539, 0759-254849, 0623-120454**

115924002


*Kwa Habari Motomoto*
*usikose Gazeti lako la*
*Nipashe kila siku*
*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

HABARI KIMATAIFA

# Trump, Biden wapambana katika mdahalo wa runinga

**WASHINGTON, Marekani**

MAHASIMU wakubwa kwenye uchaguzi mkuu wa mwezi ujao nchini Marekani, Rais Donald Trump wa Republican na Joe Biden wa Democratic, wametumia mdahalo wao wa kwanza kushambuliana.

Wawili hao wameshambuliana namna familia zao zilivyofaidika na kuwapo kwao madarakani.

Wakati Biden alipokuwa akizungumzia namna mikataba ya kibiashara ya Marekani na China isivyoleta tija iliyokusudiwa, Trump alimkatiza akitaja kuhusika kwa mtoto wa Biden, Hunter Biden, kwenye biashara nje ya nchi, hasa Ukraine.

Kwa upande wake, Biden alisema ingechukuwa usiku mzima kuzungumzia familia ya Trump, laiti angelitaka hilo.

Mbali ya mikataba ya kibiashara, mdahalo huo uliofanyika usiku wa kuamkia jana, ulitandwa pia na shutuma na tuhuma baina yao kuhusiana na masuala kadhaa, kuanzia janga la virusi vya corona, mfumo wa afya.

Mengine ni uchumi, usalama na ubaguzi wa rangi, hadi athari za mabadiliko ya tabia nchi, ambapo Biden aliahidi kuirejesha Marekani kwenye Mkataba wa Paris, ambao unalenga kupunguza uzalishaji wa gesi chafu.

DW



Rais Donald Trump na mpinzani wake wa Chama cha Democratic, Joe Biden, wakiwa kwenye mdahalo wa kwanza uliorushwa kwa njia ya luninga juzi usiku kuelekea uchaguzi wa urais utakaofanyika mwezi Novemba. **PICHA: REUTERS**

# Kesi ya kupinga uhalali wa Museveni yatupwa

**KAMPALA, Uganda**

MAHAKAMA ya Haki ya Afrika Mashariki imetupilia mbali kesi inayopinga uhalali wa Rais Yoweri Museveni, kugombea tena urais wa Uganda kwenye uchaguzi mkuu mwakani.

Wakili wa Uganda, Male Mabirizi, alikuwa amewasilisha shauri katika mahakama hiyo ya kikanda kupinga uamuzi wa mahakama ya juu zaidi ya nchi hiyo kudumisha hatua ya kufanyia marekebisho kifungu cha sheria kinachoangazia ukomo wa umri wa wagombea urais.

Marekebisho hayo yaliondoa masharti ya kumtaka mtu yeyote aliye na azma ya kuwania kiti cha urais awe na umri wa kati ya miaka 35 na 75.

Wakili Mabirizi alihoji mchakato uliyotumiwa na bunge kuidhinisha muswada wa marekebisho ya katiba mwaka 2017, hatua ambayo ilisababisha vurugu bungeni hadi kikosi maalum cha wanajeshi kupelekwa kudhibiti vurugu hizo.

Mahakama hiyo ya kikanda iliyo na makao yake mjini Arusha Tanzania, imeamua kuwa mchakato uliyotumiwa kuidhinisha muswada huo haukukiuka mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

***BBC***

# Nigeria yabuni kifaa cha kupima corona

**ABUJA, Nigeria**

NIGERIA imetengeneza kifaa ya kufanyia vipimo vya corona ambacho kina uwezo wa kutoa matokeo ya ukaguzi wa sampuli chini ya dakika 40.

Kifaa hicho kinaweza kutumiwa na watu wasiokuwa na ujuzi wa hali ya juu.

Waziri wa Afya, Olurunimbe Mamora, alisema kifaa hicho kinafanya kazi kwa haraka na bei yake ni nafuu mara 10 zaidi ya vifaa vinavyotumika sasa kufanya uchunguzi.

Kifaa hicho bado hakijaidhinishwa na mamlaka inayohusika, lakini imetoa matumaini ya nchi hiyo kuongeza juhudi za upimaji.

Mamlaka zilisema kifaa hicho kinachojulikana kama SARS-COV-2 Isothermal Molecular Assay, kilitengenezwa na Taasisi ya Utafiti wa Tiba ya Nigeria.

Hadi kufikia sasa nchi hiyo imewafanyia vipimo vya corona watu 500,000 kati ya milioni 200.

Nchi hiyo imethibitisha kuwa na watu 58,000 walioambukizwa virusi vya corona na zaidi ya vifo 1,000 huku idadi ya maambukizi ya kila siku ikipungua.

***BBC***

# Nawaf aapishwa kuwa mfalme mpya wa Kuwait

**KUWAIT CITY, Kuwait**

NAWAF al-Ahmad Al-Sabah ameapishwa kuwa mrithi wa kiti cha ufalme wa Kuwait, kama mtawala mpya wa taifa hilo la Ghuba baada ya kifo cha kaka yake, Amir Sabah al-Ahmad Al-Sabah siku ya Jumanne.

Baraza la Mawaziri la Kuwait lilimteua Nawaf mwenye umri wa miaka 83 kama mfalme mpya muda mfupi baada ya Sabah kufariki Jumanne nchini Marekani, ambako alikuwa amelazwa, akiwa na umri wa miaka 91.

Mwili wa marehemu Emir umepangiwa kuwasili nchini Kuwait jana, na msiba utahudhuriwa na ndugu tu kwa sababu ya hatua za usalama wa kiafya, kwa mujibu wa familia ya kifalme.

"Naapa kwa jina la Allah, kuheshimu katiba na sheria za nchi, kulinda uhuru wote, maslahi na mali ya umma na kulinda uhuru na mamlaka ya mipaka ya nchi," alisema mfalme huyo mpya wakati akipishwa na bunge jana.

Katika hotuba baada ya kula kiapo, Nawaf aliomboleza kifo cha mtangulizi wake, akimwelezea kama ishara ya milele, aliyeifanyia mengi nchi yake na watu wake.

"Ameacha urithi uliojaa mafanikio kwa ngazi ya kitaifa, ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.

"Taifa letu linakabiliwa na mazingira magumu katika kanda yenye machafuko, na njia pekee ya kuyamaliza haya na kuyavuka ni umoja na juhudi za pamoja."

Changamoto zinazoikabili Kuwait zinajumlisha kuwa katika kanda tete iliyoghubikwa na uhasama kati ya Saudi Arabia na Iran zina mzozo wa kidiplomasia wa miaka kadhaa kati ya kundi la mataifa linaloongozwa na Saudi Arabia dhidi ya Qatar, pamoja na kushuka kwa bei za mafuta duniani, ambayo ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya Kuwait.

Nawaf aliteuliwa kuwa mrithi wa ufalme mwaka 2006, muda mfupi baada ya Sabah kuteuliwa kuongoza.

Nawaf, ambaye alizaliwa Juni 25, mwaka 1937 katika mji mkuu wa Kuwait, alianza kazi ya siasa akiwa kwenye umri wa miaka 20, alipoteuliwa kuwa gavana wa mkoa wa Hawalli.

Nawaf baadaye alishika nyadhifa kadhaa za uwaziri, ukiwamo wa mambo ya ndani, ulinzi na masuala ya kijamii, kabla ya kuteuliwa kuwa mrithi wa kiti cha ufalme.

**BBC**




# BARCA: DEMBELE HAONDOKI NG'O

**BARCELONA, Hispania**

OUSMANE Dembele hana mpango wa kuondoka Barcelona, licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester United, kwa mujibu wa Sky Deutschland.


Dembele amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia katika Klabu ya Manchester United kabla ya dirisha la usajili kufungwa ifikapo Oktoba 5, mwaka huu.

Dembele anaonekana kuwa ndio mbadala wa Jadon Sancho, ambaye anaonekana kuwa na nafasi ndogo ya kuondoka kwa miamba wa Bundesliga, Borussia Dortmund.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania, Dembele mwenyewe hayupo tayari kuondoka pale Camp Nou.

Dembele ameonekana kuwa chaguo sahihi kwa United, ambao ni wazi kwamba wameshindwa kumsajili Sancho.

Dortmund imekataa kupunguza bei ya kumuuza Sancho na hivyo United inaona kwamba Dembele ndio chaguo sahihi kwao.



# Lampard asifia kiwango cha Mendy

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amemsifia, Edouard Mendy baada ya kucheza mechi yake ya kwanza kwa Blues kwenye Kombe la EFL, ambapo walipoteza kwa Tottenham, wakati Kepa Arrizabalaga akiwa benchi.

Mendy aliichezea kwa mara ya kwanza Chelsea baada ya kuondoka Rennes kwa ada ya pauni milioni 20 wiki iliyopita.

Akizungumzia kiwango cha Mendy, pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur, Lampard aliwaambia waandishi wa habari: "Nafikiri alikuwa vizuri. Nafikiri aliokoa hatari nyingi na kucheza vizuri sana.

"Alionyesha kuwa ana uwezo mkubwa na kiukweli atakuwa msaada mkubwa kwa timu yetu.

"Nimefurahishwa na kiwango chake na alioneka-na kama vile ameshacheza hapa kwa muda mrefu."

Erik Lamela alisawazisha bao la Timo Werner alilofunga kipindi cha kwanza kwa Chelsea na hivyo mchezo huo kulazimika kuamuliwa kwa changamoto ya penalti.

Chelsea walipoteza kwa kufungwa penalti 5-4.

# Messi ataka umoja Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi anataka kumaliza mgogoro wake na Barcelona, kwa kutaka kila mmoja klabuni hapo kuungana kwa ajili ya kuipa mafanikio klabu hiyo katika msimu huu unaoendelea.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina aliomba kuondoka pale Camp Nou Agosti, kabla ya kubadilisha uamuzi wa kubakia klabuni hapo.

Messi alifungwa kwa penalti katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu, wakati Ronald Koeman akiiongoza kwa mara ya kwanza timu hiyo, dhidi ya Villarreal pale Camp Nou.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Messi alisema kwa sasa anataka kila mmoja kuungana kwenye klabu hiyo kwa ajili ya kutafuta mafanikio.

"Baada ya mambo mengi, ningependa kumaliza kila kitu hapa. Tunatakiwa kuungana, ili kuhakikisha timu inakuwa na mafanikio kwa msimu huu," alisema mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

"Kwa sasa mimi akili yangu ni kutaka Barcelona iwe na mafanikio makubwa msimu huu na kuifanya kuwa imara zaidi."



## HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA SASA KUSAJILI BEKI TU

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anajiandaa kutumia kiasi cha pauni milioni 390, kwa ajili ya kusajili mabeki kabla ya kufungwa kwa pazia la usajili.

Tayari amesham- sa mlinzi wa kimataifa na kati wa wa Ureno, Ruben Dias kutoka Benfica kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 64.5.

Uhamisho huo utamshuhudia Nicolas Otamendi akitimkia Benfica kwa ada ya pauni milioni 13.7 baada ya klabu hizo mbili kukubaliana.

Licha ya kwamba Vincent Kompany alikuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara kwenye miaka yake michache ya mwishoni kwenye klabu hiyo, bado ameacha pengo ambalo limeshindwa kuzibwa tangu alipoondoka Mei 2019.

City hadi sasa imetumia zaidi ya pauni milioni 105 kunasa mabeki wa kati pekee, Dias na Nathan Ake.

Mtangulizi wake, Manuel Pellegrini fedha kubwa aliyotumia kwenye beki ni ile pauni milioni 30 alizolipa kupata huduma za Otamendi na Eliaquim Mangala.

Hata hivyo, bado inaonekana ni ngumu kuamini kama ujio wa Dias utamaliza tatizo la mabeki kwenye kikosi hicho cha Etihad.

Usajili wa mabeki wa kati, ambao wamesajiliwa na Guardiola hapo City na kumgharimu pauni milioni 390 ni John Stones kutoka Everton, Kyle Walker kutoka Tottenham Hotspur, Danilo, Aymeric Laporte.

## PEREIRA ASAJILIWA LAZIO KWA MKOPO

**ROME, Italia**

KIUNGO mshambuliaji wa Manchester United, Andreas Pereira amekubali kujiunga na Lazio kwa mkopo wa msimu mzima.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na United mwaka 2014, lakini hadi sasa ameshindwa kulishawishi benchi la United kumpa nafasi ya kucheza.

Hata hivyo, kwa kipindi chote hicho alikuwa akikitumikia kikosi cha Granada na Valencia kwa mkopo katika nyakati tofauti.

Katika msimu wa kwanza wa kocha Ole Gunnar Solskjaer alionekana anaenda kuwa chaguo la kwanza, ambapo alicheza mechi 40 katika msimu wa mashindano.

Lakini baadaye akaonekana kutopata namba kwenye kikosi hicho na hivyo klabu yake hiyo imeamua kumtoa kwa mkopo tena.

# Zidane: Hazard aimarika, akaribia kurudi dimbani

**MADRID, Hispania**

EDEN Hazard anakaribia kurudi kwenye ufiti wake huku kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane akikanusha taarifa kwamba fowadi huyo amekosa weledi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amejikuta kwenye wakati mbaya nchini Hispania baada ya kutua pale kwa euro milioni 100 kutoka Chelsea Juni, mwaka jana.


Zidane alidokeza kwamba, Hazard yupo tayari kurudi uwanjani kwa mara ya kwanza msimu huu.

"Nafikiri anakaribia kurudi dimbani," alisema Zidane. "Amejiandaa vizuri na anafanya mazoezi ya timu vizuri.

"Ishu ni kwamba hajaweza kufanya mazoezi kwa kiwango kikubwa hadi sasa, lakini amerudi kwenye mazoezi. Hivyo tutaona nini kitatokea.

"Anachotaka ni kucheza. Alikuwa na tatizo kubwa lililomfanya awe nje ya dimba kwa muda mrefu, lakini sasa anaonekana kuwa fiti.

"Msimu ni mrefu na yeye ana weledi. Ni mchezaji wa aina yake anayejitambua na anajua nini anapaswa kufanya."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YATARAJIA MAZURI KWA JOVIC

●●●Yawasilisha ofa ya kumsajili mshambuliaji huyo ambaye anatajwa kutokuwa kwenye...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inaamini ikifanikiwa kumsajili Luka Jovic itakuwa imeimarisha kikosi chake baada ya Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, kuonyesha kutombubali straika huyo ambaye amepata baraka za kuondoka na kujiunga na klabu nyingine kwa mkopo.

Kwa mujibu wa gazeti la MailOnline, United imewasilisha ofa ya kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Serbia mwenye umri wa miaka 22, kutoka kwa mabingwa hao wa Hispania.

Zidane alisema milango iko wazi kwa anayetaka kumsajili straika huyo, ambaye tayari United imeonyesha nia ya kumsajili ingawa klabu nyingine za Italia ikiwamo Inter, AC Milan na Roma pia zinamwinda.

Alipoulizwa kuhusu Jovic katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi ya La Liga dhidi ya Real Valladolid iliyochezwa juzi usiku, Zidane alisema: "Inahitaji kuhakikisha kila jambo sawa sawa, ila tusubiri hadi Oktoba 5, kwa sasa yuko sokoni.

"Tutaangalia. Wachezaji wako vizuri na kwamba kile kinachonivutia."

Mshambuliaji huyo alijiunga na Madrid mwaka jana akitokea Eintracht Frankfurt kwa dau la pauni milioni 55, lakini akiwa hapo amefunga mabao mawili kwenye mechi 28 alizocheza huku akikabiliwa na majeruhi.

Nyota huyo alianza katika mechi nne tu za La Liga msimu uliopita na kufunga magoli hayo mawili, ikiwa ni tofauti ya kiwango cha juu alichokionyesha katika mwaka wake wa mwisho alipokuwa kwenye Ligi ya Ujerumani maarufu Bundesliga.

Msimu wake wa mwisho akiwa Frankfurt, alifanikiwa kufunga mabao 27, yakiwamo 10 yaliyowapeleka kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa, mchezo ambao alishuhudia wakipoteza kwa kufungwa na Chelsea. Tottenham pia ilikuwa kwenye mchakato wa kumsajili Jovic wakati wa mazungumzo ya kuwanasa, Gareth Bale na Sergio Reguilon hayajakamilika, lakini kwa sasa wameshamalizana na nyota hao.

United imeendelea kujipanga kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, lakini, kanuni za fedha zinawabana katika kuamua hatima ya saini ya winga huyo anayecheza soka nchini Ujerumani.

## KWA UFUPI

### DORTMUND YAIBANIA UNITED
MANCHESTER United imeendelea kuwa njia panda baada ya ofa yake ya pauni milioni 91.3 ya kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), kukataliwa na klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Sports)***

### DEMBELE KUTUA UNITED
MANCHESTER United inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(AS- in Spanish)***

### DEPAY ANUKIA BARCA
BARCELONA inatarajia kutumia fedha itakazopata kwa kumuuza Ousmane Dembele, kufanikisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Lyon na nyota wa zamani wa Manchester United, Memphis Depay. ***(AS - in Spanish)***

### GUARDIOLA ATAKA WAWILI
KOCHA Pep Guardiola anataka kumsajili beki wa kushoto mpya kabla ya dirisha la usajili halijafungwa huku nyota wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba, mchezaji wa Ajax na Argentina, Nicolas Tagliafico wote wakiwa kwenye orodha ya wachezaji wanaotakiwa na klabu hiyo ya Manchester City. ***(Mail)***

### LAMPTEY ATAJWA BAYERN
MABINGWA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich wameanza mazungumzo na Brighton kwa ajili ya kumsajili beki wa kulia wa timu hiyo ambaye ni raia wa England, Tariq Lamptey. ***(Sport1, via Metro)***

### CUISANCE KUTUA LEEDS
LEEDS United inakaribia kukamilisha usajili wa kiungo Mfaransa wa Bayern Munich, Michael Cuisance (21), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni tisa. ***(Athletic - subscription required)***

### KOLASINAC SOKONI
BAYER Leverkusen imewasilisha ofa ya milioni tisa ili kumsajili beki wa kushoto wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Bosnia, Sead Kolasinac (27), kwa dau la pauni milioni tisa. ***(Mail)***

### VEERMAN ANUKIA EPL
KLABU ya Southampton inatarajia kupeleka ofa ya kumsajili kiungo wa Heerenveen na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Joey Veerman, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Voetbal International, via TalkSPORT)***

### TORREIRA ATAJWA ATLETICO
WAKALA wa Lucas Torreira ametua jijini Madrid kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Atletico Madrid kuhusiana na uhamisho wa nyota huyo wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Uruguay kujiunga na klabu hiyo ya Hispania. ***(Fabrizio Romano, via Express)***

### RUDIGER NJIA NYEUPE
CHELSEA iko tayari kumuuza beki wake Mjerumani, Antonio Rudiger (27), ambaye anawindwa na Tottenham, lakini itafurahi zaidi ikiona nyota huyo anajiunga na klabu nyingine ya nje ya England. ***(ESPN)***

### WEST HAM YAKWAMA
OFA ya mkopo ya West Ham inayohitaji huduma ya beki wa kulia wa Slavia Prague na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Czech, Vladimir Coufal (28), imekataliwa. ***(90min)***

# TFF, MALYA WAKUBALIANA KUWANOA WADAU NCHINI

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesaini mkataba wa kudumu na Chama cha Maendeleo ya Michezo cha Malya kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa mchezo huo hapa nchini.

Halfa ya kusaini mkataba huo ilifanyika sambamba na uzinduzi wa Kituo cha Maendeleo ya Michezo cha Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema mkataba huo utasaidia kupeleka wataalamu wao kujifunza mbinu za kusimamia vyema maendeleo ya michezo mbalimbali hapa nchini.

Karia alisema ilikuwa ni moja ya sera zake wakati anaingia madarakani kuhakikisha Tanzania inakuwa na Chuo cha Michezo ili kuwaandaa viongozi waadilifu na kila idara inakuwa na viongozi wenye weledi.

"Mkataba huu una faida kubwa kwa sababu utatusaidia kupata wataalamu mbalimbali pamoja na kutoa ajira kwa wadau wa michezo ambao watakuwa wamepata mafunzo ya hali ya juu," alisema Karia.

Rais huyo aliwataka wasemaji wa klabu mbalimbali hapa nchini kushiriki kozi inayohusiana na kazi wanayoifanya ili wafahamu vyema namna ya kutekeleza majukumu yao na kuacha 'kupiga porojo' huku akielekeza timu kuajiri maofisa ambao wanaujua vizuri mchezo wa soka.

"Tunataka wasemaji wapigwe msasa ili wajue wajibu wao, kuliko kuwa na wasemaji ambao hawajui wajibu wao ndani ya klabu, tukiwa na wasemaji wajuzi kila kitu kitakuwa kinakwenda kisasa hatutaki porojo," Karia alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hassan Abbas, alitoa siku 60 kwa vyama vyote vya michezo nchini kuingia mkataba na chuo hicho ili kuwajenga katika kazi zao.

Abass alisema mkataba ambao umesainiwa una thamani kubwa hivyo, wadau hao wa michezo wanatakiwa kutopoteza fursa ya kupata mafunzo.

Aliongeza serikali imeahidi kushirikiana na vyama vyote vya michezo nchini ili kuinua viwango vya michezo.



Wanachama wa klabu mbalimbali za Jogging, Dar es Salaam wakishiriki bonanza maalumu lililoandaliwa na Benki ya Diamond Trust Bank, Jubilee Life Insurance na Aga Khan ambalo lilifanyika kwenye Viwanja vya Tanganyika Packers jijini Jumapili iliyopita. Bonanza hilo lilizinduliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Raundi nne zachezwa bila penalti

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 inatarajia kuendelea kesho, raundi nne yenye mechi 36 imechezwa huku kukiwa hakuna penalti iliyotolewa ingawa bao moja tu la kujifunga limepatikana.

Jumla ya magoli 54 yamefungwa mpaka sasa katika ligi hiyo yenye timu 18.

Hii ni tofauti kidogo na msimu uliopita ambapo mpaka raundi nne zinakamilika mabao 58 yalikuwa yamepatikana, penalti moja na magoli mawili ya kujifunga.

Kwa mujibu wa rekodi zilizopo ni kwamba mpaka sasa zimechezwa jumla ya mechi 36, mechi za ushindi zikiwa 29 na sare saba.

Pia rekodi zinaonyesha kuwa mechi ambazo timu zimeshinda nyumbani ni 18, huku mechi za timu kushinda ugenini zikiwa 11 na sare za jumla zikiwa saba, kukiwa na magoli yote 54 ambayo yote yamefungwa kwa njia ya kawaida.

Bao pekee la kujifunga kwenye ligi mpaka sasa ni la Edson Katanga wa JKT Tanzania, alipouweka mwenyewe wavuni mpira Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, timu yake ikipoteza bao 1-0 dhidi ya Coastal Union.

Msimu uliopita, hadi kufikia raundi ya nne tayari magoli yalishafika 58 na magoli mawili ya kujifunga, Ibrahim Said wa Mbao FC, akijifunga kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Alliance FC na kutoka sare ya bao 1-1, huku George Chota wa Mbeya City akijifunga kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Ruvu Shootinga, timu hizo zikitoka sare ya goli 1-1.

Penalti iliyopatikana msimu uliopita mpaka kufikia raundi ya nne ilikuwa ni kati ya Simba dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, ikifungwa na Meddie Kagere, akiisaidia timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0.

## JKT Stars, Oilers majaribuni Dar

**Na Adam Nyangasa, TUDARCo**

TIMU ya JKT Stars inatarajia kuvaana na Oilers katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kikapu ya Mkoa wa Dar es Salaam itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kurasini, jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Chama cha Mpira wa Kikapu Dar es Salaam (DARBA), Daniel Kapongo, alisema timu zote mbili zimejiandaa vyema na mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani.

Kapogo alisema wamepanga mchezo huo kufanyika kuanzia saa 12:00 jioni na maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika.

"Mashindano yetu yameingia katika hatua ya nusu fainali, hatua hiyo inahusisha timu za wanawake na wanaume, na mechi zao zitachezwa kwa wakati mmoja," alisema Kapogo.

Kiongozi huyo alisema mchezo mwingine wa hatua ya nusu fainali utakuwa ni kati ya ABC dhidi ya Kurasini Heat na utaanza kuchezwa kuanzia saa 2: 00 usiku.

Alizitaja timu za wanawake zilizotinga hatua hiyo ni pamoja na Ukonga Queens, Vijana Queens, Don Bosco Lioness na JKT Stars.

## Kikwajuni yaahidi kurejesha makali

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UONGOZI wa Kikwajuni umesema wanajipanga kuhakikisha timu yao inafanya vyema kwenye Ligi Daraja la Pili msimu ujao wa 2020/21 na hatimaye kupanda daraja katika msimu unaofuata.

Msimu uliopita, Kikwajuni haikuwa na msimu mzuri na hatimaye kushuka daraja katika Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kikwajuni, Juma Abdallah Juma, alisema msimu matokeo mabaya waliyopata katika msimu uliopita, yalitokana na kushindwa kujipanga vizuri.

Juma alisema hawakusajili kikosi chenye ushindani na hivyo walishindwa kukabiliana na changamoto mbalimbali walizokutana nazo.

**"Hatukuwa na msimu mzuri wa 2019/20, hatukujipanga vizuri, tulisajili wachezaji wenye viwango ambavyo haviwezi kuhimili kishindo cha Ligi Daraja la Kwanza, tunatarajia kuanza mazoezi wiki hii kwa ajili ya kujiweka imara," alisema kiongozi huyo.**

Aliongeza hawatarudia makosa hayo na msimu huu watasajili wachezaji watakaoisaidia timu hiyo na watafuata mapendekezo yatakayotolewa na kocha wa timu hiyo.

Michezo
Alhamisi Oktoba 1, 2020
Nipashe



## UNITED YATARAJIA MAZURI KWA JOVIC

HABARI UK 22

## CHAMA, MUGALU KULINDWA SIMBA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI mikataba ya baadhi ya wachezaji nyota wa kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ikibakiza muda mfupi, uongozi wa klabu hiyo umesema 'utawalinda' mastaa wake ili wasiondoke klabuni hapo kirahisi.

Kauli hiyo imesemwa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Haji Manara, ambaye alitembelea ofisi za gazeti hili zilizopo Mikocheni jijini, Dar es Salaam juzi.

Manara alisema Simba imeanza mazungumzo na wachezaji wake ambao mikataba yao inaelekea ukingoni na hakuna mchezaji ambaye watamhitaji kubakia klabuni hapo, wakashindwa kutekeleza mahitaji yake.

Alisema mazungumzo na nyota hao yako katika hatua nzuri kwa sababu wanataka kuendelea kuwa na kikosi imara kitakachowapeleka kwenye hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aliwataja baadhi ya nyota ambao mazungumzo yameanza ni pamoja na kiungo Mzambia, Clatous Chama na mshambuliaji kutoka Rwanda, Meddie Kagere.

"Niwatoe hofu mashabiki na wanachama wa Simba, hakuna mchezaji atakayeondoka bila klabu kutaka, wachezaji wote ambao tupo kwenye mazungumzo nao tumefikia hatua nzuri na wote watabaki, nisemu wazi Simba tumejipanga kuwalinda nyota wetu," alisema Manara.

Aliongeza kwa hali ya sasa hakuna mchezaji ambaye ataondoka Simba na kutua klabu nyingine hapa nchini kama alikuwa kwenye malengo yao.

"Simba tuna malengo ya kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa, hivyo ni lazima tuwe na kikosi imara na kwa hapa nyumbani mchezaji wetu ataenda timu gani? Labda kama tutake kumwachia," alisema Manara.

Aliwaondoa hofu mashabiki na wanachama wa timu hiyo kwamba viongozi wao wamejipanga kutorudia makosa ya miaka ya nyuma na kueleza winga wao, Luis Miquissone, bado ana mkataba mrefu na klabu hiyo.




Kiungo wa Chelsea, Mason Mount (kushoto), akishindwa kufunga baada ya mpira aliopiga kugonga mwamba huku kipa wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris, akiruka kujaribu kuokoa shambulizi hilo katika mechi ya Kombe la Ligi iliyochezwa juzi usiku. Spurs ilishinda penalti 5-4. **PICHA: MTANDAO**

# AZAM ANGA MOJA NA SIMBA, YANGA

●●●Yatambia safu yake ya ushambuliaji, ikimtaja Prince Dube anakaribia kuchukua ufalme...

**Na Saada Akida**

SAFARI ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu inaonekana kuwa na ushindani zaidi baada ya benchi la ufundi la Azam FC kujipanga kupambana na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga kuwania taji hilo, imefahamika.

Azam FC yenye pointi 12, ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushinda mechi zote nne walizocheza, wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba na Yanga zenye pointi 10 kila moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema msimu huu wanaamini kikosi chao kina nafasi ya kutwaa ubingwa kutokana na kuwa na safu imara na nzuri ya ushambuliaji.

Vivier alisema kila mchezaji wa Azam FC, amejiandaa kuonyesha kiwango cha juu katika kila mechi ili kuhakikisha wanapambana kupata matokeo chanya kwenye mechi zote watakazocheza.

"Msimu huu tuko kwenye mbio za ubingwa, tunajivunia safu bora ya washambuliaji tuliyokuwa nayo, kila mshambuliaji atakayecheza anaweza kufunga na kuibuka na ushindi, hii inatujenga na kutuweka mahali salama," alisema Vivier.

Mrundi huyo alisema msimu huu wana kikosi bora ukilinganisha na cha msimu uliopita ambapo katika safu ya ushambuliaji walikuwa wakimtegemea zaidi, Obrey Chirwa ambaye ndio alikuwa kinara wa wafungaji ndani ya timu yao hiyo.

"Tumejipanga kuleta ushindani mkubwa, ukiangalia safu ya ushambuliaji imekuwa na mabadiliko tofauti na msimu uliopita, imani yetu tunapambana kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi tunazocheza za nyumbani na ugenini pia," alisema Vivier.

Aliongeza kikosi chao kinaendelea na maandalizi ya kujiwinda na mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar itakayopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri, hasa wakicheza katika uwanja wa nyumbani.

Kocha huyo alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu ya timu zote zinahitaji kupata matokeo, wao wakihakikisha wanaendeleza rekodi yao ya ushindi wakati Kagera Sugar iliyoanza msimu kwa 'kusuasua' ikitaka kujiondoka mkiani.

"Kiwango cha Prince Dube kwetu ni faraja, amekuwa akionyesha yeye ni mshambuliaji halisi, anaisaidia timu kupata matokeo na amekuwa na mchango mkubwa kwenye mechi zote tulizocheza, tumepata pacha wa Chirwa, tunaamini tutakuwa na msimu mzuri," Vivier alisema.

Dube anaongoza katika orodha ya wafungaji akiwa na mabao matatu, akifuatiwa na Clatous Chama, Meddie Kagere, Chris Mugalu, Muzamiru Yassin wote kutoka Simba, Hassan Kabunda, Reliant Lusajo (KMC), Marcel Kaheza (Polisi Tanzania), Lamine Moro (Yanga) na Bigirimana Blaise wa Namungo FC.

Azam FC itaikaribisha Kagera Sugar katika mechi ya raundi ya tano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >